# MAELEKEZO KWA VYAMA VYA SIASA NA WAGOMBEA

## YALIYOMO


UJUMBE WA MWENYEKITI ........ vii

DIBAJI ........ viii

TAFSIRI YA MANENO ........ ix

SURA YA KWANZA ........ 1

UTEUZI WA WAGOMBEA ........ 1

1.1. Siku ya Uteuzi ........ 1

1.2. Mamlaka za Uteuzi ........ 1

1.3. Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea Wakati wa Uteuzi ........ 2

1.4. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Zaidi ya Mmoja ........ 4

1.5. Daftari na Orodha ya Wapiga Kura ........ 5

SURA YA PILI ........ 7

UTEUZI WA MGOMBEA WA KITI CHA RAIS NA MAKAMU WA RAIS ........ 7

2.1. Sifa za Mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ........ 7

2.2. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ........ 7

2.3. Masharti ya Urejeshaji wa Dhamana za Wagombea ........ 8

2.4. Fomu za Uteuzi (Fomu Na. 8A) ........ 9

2.5. Wadhamini wa Wagombea ........ 9

2.6. Uthibitisho wa Msimamizi wa Uchaguzi Juu ya Wadhamini ........ 10

2.7. Uwasilishaji Rasmi wa Fomu za Uteuzi ........ 10

2.8. Uthibitisho wa Tume Kuwateua Wagombea ........ 12

2.9. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais ........ 13

2.10. Uamuzi wa Tume ........ 15

2.11. Kutokuwepo au Kufariki kwa Mgombea ........ 16

2.12. Mgombea Pekee wa Kiti cha Rais ........ 16

2.13. Kujitoa kwa Mgombea ........ 16

SURA YA TATU ........ 18

UTEUZI WA MGOMBEA UBUNGE ........ 18

3.1. Sifa za Mgombea Ubunge ..... 18
3.2. Kukosa Sifa za Kugombea Ubunge ..... 18
3.3. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge ..... 20
3.4. Masharti ya Urejeshaji wa Dhamana za Wagombea ..... 21
3.5. Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8B) ..... 21
3.6. Utoaji wa Fomu za Uteuzi ..... 22
3.7. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi ..... 24
3.8. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Ubunge Zaidi ya Mmoja ..... 25
3.9. Kubandika Fomu za Uteuzi wa Wagombea Ubunge ..... 25
3.10. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge ..... 26
3.11. Utaratibu wa Msimamizi wa Uchaguzi kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea ..... 29
3.12. Utaratibu wa Kukata Rufaa ..... 30
3.13. Uamuzi wa Tume ..... 30
3.14. Kutokuwepo kwa Wagombea ..... 31
3.15. Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa ..... 31
3.16. Kujitoa kwa Mgombea ..... 31
3.17. Kufariki kwa Mgombea ..... 32
**SURA YA NNE ..... 33**
**UTEUZI WA WAGOMBEA UDIWANI ..... 33**
4.1. Sifa za Mgombea Udiwani ..... 33
4.2. Kukosa Sifa za Kugombea Udiwani ..... 33
4.3. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani ..... 34
4.4. Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8C) ..... 35
4.5. Utoaji wa Fomu za Uteuzi ..... 36
4.6. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi ..... 37
4.7. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Udiwani Zaidi ya Mmoja ..... 38
4.8. Kubandika Fomu za Uteuzi wa Wagombea Udiwani ..... 39
4.9. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani ..... 40
4.10. Utaratibu wa Kuwasilisha Rufaa ..... 44

4.11. Uamuzi wa Tume ... 45
4.12. Kutokuwepo kwa Wagombea ... 45
4.13. Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa ... 45
4.14. Kujitoa kwa Mgombea ... 45
SURA YA TANO ... 45
UTARATIBU WA WATUMISHI WA UMMA KUGOMBEA UBUNGE NA UDIWANI ... 46
5.1. Wanaoruhusiwa na Wasioruhusiwa Kugombea Miongoni mwa Watumishi wa Umma ... 46
5.2. Wakati wa Kujitayarisha Kugombea ... 47
5.3. Baada ya Kuteuliwa au Kutangazwa na Tume ... 47
SURA YA SITA ... 49
KAMPENI NA MAADILI YA UCHAGUZI ... 49
6.1. Kipindi cha Kampeni ... 49
6.2. Wajibu wa Vyama vya Siasa, Wagombea na Mawakala ... 49
6.3. Wajibu wa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Kata katika Kuratibu Ratiba za Kampeni za Wagombea Ubunge na Udiwani ... 51
6.4. Utaratibu wa Kubadili Ratiba ya Kampeni ... 52
6.5. Maelekezo ya Jumla ... 52
6.6. Maadili ya Uchaguzi ... 53
SURA YA SABA ... 55
UPIGAJI KURA ... 55
7.1. Vituo vya Kupigia Kura na Uteuzi wa Watendaji wa Vituo ... 55
7.2. Haki ya Vyama vya Siasa na Wagombea Kuteua Mawakala ... 56
7.3. Utambulisho wa Mawakala wa Vyama Vya Siasa ... 56
7.4. Kiapo cha Kutunza Siri kwa Mawakala ... 58
7.5. Mafunzo kwa Mawakala ... 58
7.6. Wajibu wa Mawakala ... 59
7.7. Vyama au Wagombea Kushuhudia Ugawaji wa Vifaa ... 60
7.8. Wanaoruhusiwa Kuingia Ndani ya Kituo cha Kupigia Kura ... 60

7.9. Matumizi ya Fomu Na. 15 na Fomu Na. 17 ... 62

7.10. Vibali vya Watendaji wa Uchaguzi, Mawakala na Wagombea ... 63

7.11. Mambo Yasiyoruhusiwa Kufanyika Siku ya Kupiga Kura ... 64

**SURA YA NANE** ... 65

**KUHESABU KURA** ... 65

8.1. Utaratibu wa Kuhesabu Kura ... 65

8.2. Wanaoruhusiwa Kuwepo Wakati wa Kuhesabu Kura ... 66

8.3. Matokeo ya Uchaguzi katika Kituo ... 67

**SURA YA TISA** ... 69

**KUJUMLISHA KURA** ... 69

9.1. Wanaoruhusiwa Kuingia katika Kituo cha Kujumlisha Kura ... 69

9.2. Utaratibu wa Kufuata Kabla ya Kuanza Kujumlisha Kura ... 70

9.3. Utaratibu wa Kufuata Wakati wa Kujumlisha Kura ... 70

9.4. Kujumlisha Kura za Uchaguzi wa Rais na Wabunge ... 71

9.5. Matokeo ya Uchaguzi wa Rais katika Jimbo ... 72

9.6. Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge katika Jimbo ... 72

9.7. Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani katika Kata ... 73

9.8. Maombi ya Wakala au Mgombea Kurudia Kuhesabu Kura ... 73

9.9. Kujumlisha Kura za Uchaguzi wa Rais kwa Nchi Nzima ... 74

9.10. Yanayotakiwa Kufanywa na Tume Kabla ya Kuanza Ujumlishaji wa Kura za Rais ... 74

9.11. Kumtangaza Mshindi wa Kiti cha Rais ... 75

**SURA YA KUMI** ... 76

**UTEUZI WA WABUNGE NA MADIWANI WA VITI MAALUM VYA WANAWAKE** ... 76

10.1. Wabunge wa Viti Maalum vya Wanawake ... 76

10.2. Madiwani wa Viti Maalum vya Wanawake ... 77

**SURA YA KUMI NA MOJA** ... 79

**USHAURI KWA VYAMA VYA SIASA** ... 79

**UJUMBE WA MWENYEKITI**

Vyama vya Siasa ni wadau muhimu katika shughuli za Uchaguzi. Kwa mujibu wa Sheria za nchi yetu ili mtu akubalike kuwa mgombea ni lazima awe amedhaminiwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu. Tume ya Taifa ya Uchaguzi huteua wagombea wa nafasi ya kiti cha Rais, Ubunge na Madiwani baada ya kupata barua za utambulisho kutoka kwenye vyama vya siasa.

Tume imejiwekea utaratibu wa kuvishirikisha vyama vya siasa katika mchakato mzima wa uendeshaji wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ili kuweka uwazi katika uchaguzi. Tunatarajia kupata ushirikiano kutoka kwa vyama vya siasa na wagombea ili kuhakikisha kuwa Uchaguzi Mkuu unafanyika kwa amani na utulivu.

Vyama vya siasa vinashauriwa kuhamasisha wanachama kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi. Wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ni makundi muhimu ambayo inashauriwa yapewe fursa ya kushiriki katika nafasi za uongozi.

JAJI WA RUFAA (MST.) SEMISTOCLES S. KAIJAGE
*Mwenyekiti*
*Tume ya Taifa ya Uchaguzi*

## DIBAJI

Maelekezo haya yanalenga kuviwezesha vyama vya siasa na wagombea kuyaelewa mambo ya msingi kuhusiana na hatua mbalimbali za uchaguzi.

Viongozi wa vyama vya siasa na wagombea wanapaswa kusoma maelekezo haya na kuyaelewa ipasavyo ili waweze kutekeleza wajibu wao vizuri katika hatua zote za mchakato wa uchaguzi hususan kwenye hatua za uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi, kupiga kura, kuhesabu kura, kujumlisha kura na kutangaza matokeo. Vile vile, ili kupata uelewa zaidi wanatakiwa kuzisoma na kuzielewa Sheria za Uchaguzi, Kanuni na Maelekezo yote yaliyotolewa na Tume.

Nawasihi kutoa ushirikiano kwa Tume na Wasimamizi wa Uchaguzi katika hatua zote za uendeshaji wa Uchaguzi.

DKT. WILSON MAHERA CHARLES
**Mkurugenzi wa Uchaguzi**

## TAFSIRI YA MANENO

Kwa madhumuni ya Maelekezo haya: -

**1. Tume**

Ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliyoundwa kwa mujibu wa ibara ya 74 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.

**2. Chama cha Siasa**

Ni chama kilichopata usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura ya 258.

**3. Mgombea**

Ni mtu aliyependekezwa na chama cha siasa aliyetimiza masharti ya uteuzi ili achaguliwe kwenye uchaguzi wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge au Udiwani.

**4. Wakala**

Ni mwakilishi aliyeteuliwa na chama cha siasa baada ya kupata ridhaa ya mgombea kwa ajili ya kusimamia maslahi ya chama na/au mgombea katika uchaguzi.

**5. Pingamizi dhidi ya Uteuzi wa Mgombea**

Ni haki ya kusema kwamba mgombea yeyote aliyeteuliwa na Tume aondelewe kuwa mgombea kwa sababu hana sifa stahiki za kuwa mgombea kwa mujibu wa sheria.

# SURA YA KWANZA

## UTEUZI WA WAGOMBEA

### 1.1. Siku ya Uteuzi

Kwa mujibu wa vifungu vya 32 (1), (2) na (3) na 37 (1) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 41 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 siku ya uteuzi ni siku iliyotangazwa na Tume kuwa ndiyo siku ambayo wagombea watawasilisha fomu za uteuzi. Fomu hizo sharti ziwasilishwe si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni. Watendaji wa uchaguzi watakuwepo ofisini kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa kumi kamili (10:00) jioni kukamilisha zoezi hilo.

### 1.2. Mamlaka za Uteuzi

Mamlaka zitakazoshughulikia uteuzi wa wagombea ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Mgombea | Mamlaka ya Uteuzi |
|---|---|---|
| (i) | Mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais | Tume ya Taifa ya Uchaguzi |
| (ii) | Mgombea Ubunge | Msimamizi wa Uchaguzi |
| (iii) | Mgombea Udiwani | Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata |

## 1.3. Wajibu wa Vyama vya Siasa na Wagombea Wakati wa Uteuzi

### (i) Wajibu wa Vyama vya Siasa

Vyama vya siasa vitakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kupendekeza wagombea wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria.

(b) Kuwatambulisha wagombea kwenye mamlaka za uteuzi kwa barua. Mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, barua yao ya utambulisho iandikwe na Katibu Mkuu wa chama, mgombea Ubunge barua yake iandikwe na Katibu wa chama wa jimbo, wilaya au mkoa na kwa mgombea Udiwani, barua iandikwe na Katibu wa chama wa wilaya, jimbo au kata.

(c) Kuwathibitisha wagombea waliowapendekeza kwa kuweka saini kwenye fomu za uteuzi za wagombea husika.

(d) Vyama ambavyo vina mgawanyiko wa uongozi vihakikishe kwamba: -

i. Fomu za mgombea Ubunge zinasainiwa na viongozi wa kitaifa wanaotambuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa.

ii. Fomu za mgombea Udiwani zisainiwe na uongozi wa mkoa, wilaya au jimbo unaotambuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa.

**(ii) Wajibu wa Wagombea**

Wagombea watakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kuchukua, kujaza na kurudisha fomu za uteuzi.

(b) Kuhakikisha na kujiridhisha kwamba wanazo sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Uchaguzi, na kwamba hawajapoteza sifa yoyote.

(c) Kuelewa vema aina za fomu zinazohitajika katika zoezi la uteuzi, masharti ya uteuzi na mahali ambapo wanaweza kuzipata fomu hizo. Pia, wanatakiwa kufahamu tarehe, mahali na masharti ya kuzirejesha fomu hizo.

i. Fomu kwa ajili ya uteuzi zitapatikana kama ifuatavyo:-

- Fomu za wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais zitapatikana Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
- Fomu za wagombea Ubunge zitapatikana kwa Msimamizi wa Uchaguzi, na
- Fomu za wagombea Udiwani zitapatikana kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata.

ii. Urejeshwaji wa fomu za uteuzi utakuwa kama ifuatavyo:-

- Fomu za wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais zitarejeshwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi,

- Fomu za wagombea Ubunge zitarejeshwa kwa Msimamizi wa Uchaguzi, na
- Fomu za wagombea Udiwani zitarejeshwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata.

(d) Kupata wadhamini kwa idadi inayohitajika.

Ifahamike kwamba mpiga kura mmoja anaweza kumdhamini mgombea mmoja tu kwa uchaguzi wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge na Udiwani. Wadhamini wanatakiwa kujaza taarifa zao katika nakala zote nne za fomu za mgombea.

(e) Kusaini fomu ya kukubali na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 mbele ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi kwa wagombea Ubunge na mbele Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kwa wagombea Udiwani siku ya uteuzi.

**Ushauri**:

Tume inashauri mapendekezo ya uteuzi wa wagombea yazingatie uwiano wa jinsia na makundi maalum kama vile watu wenye ulemavu na vijana.

### 1.4. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Zaidi ya Mmoja

Mpiga kura atatakiwa kumdhamini mgombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais, Ubunge au Udiwani mmoja tu katika uchaguzi unaohusika. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 38 (9) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 42 (9) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Endapo atadhamini mgombea zaidi ya mmoja na wagombea hao wakateuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata, udhamini huo hautabatilisha uteuzi wao, isipokuwa itakuwa ni kosa la kiuchaguzi kwa mpiga kura huyo kwa mujibu wa kifungu cha 38 (11) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 42 (11) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

Utaratibu wa kushughulikia mpiga kura aliyedhamini zaidi ya mgombea mmoja utakuwa kama ifuatavyo: -

(i) Kwa mujibu wa kifungu cha 38 (11) na (12) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 42 (11) na (12) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mpiga kura aliyedhamini mgombea zaidi ya mmoja akikubali kosa kwa maandishi, Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kutoa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki mbili (200,000/=).

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa atoe stakabadhi ya malipo pale mdhamini anapolipa fedha hizo.

(iii) Mpiga kura asipokubali kosa kwa maandishi shauri hili litapelekwa Mahakamani.

### 1.5. Daftari na Orodha ya Wapiga Kura

Tume itatoa nakala tete (*soft copy*) ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa vyama vya siasa. Vyama vya siasa vinaweza kuwapatia nakala ya daftari hilo mawakala wao siku ya uchaguzi. Hata hivyo, Daftari rasmi litakalotumika Siku ya

Uchaguzi katika kila kituo ni lile litakalotolewa na Msimamizi wa Uchaguzi.

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litaonesha wapiga kura wanaoruhusiwa kupiga kura katika kituo cha kupigia kura.

Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kila kituo litakuwa na idadi ya wapiga kura itakayoelekezwa na Tume na litaonesha taarifa zifuatazo kwa kila mpiga kura:-

(a) Jina kamili la mpiga kura.

(b) Jinsi.

(c) Tarehe na mwaka wa kuzaliwa.

(d) Picha ya mpiga kura.

(e) Namba ya mpiga kura.

## SURA YA PILI

## UTEUZI WA MGOMBEA WA KITI CHA RAIS NA MAKAMU WA RAIS

### 2.1. Sifa za Mgombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Endapo mgombea wa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano atatoka sehemu moja ya Muungano, mgombea wa nafasi ya Makamu wa Rais atatoka sehemu ya pili ya Muungano.

Kwa mujibu wa ibara ya 39(1) na 47(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, sifa za mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ni zifuatazo: -

(i) Awe raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa sheria ya uraia;

(ii) Awe ametimiza umri wa miaka arobaini;

(iii) Awe ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;

(iv) Awe na sifa za kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi; na

(v) Katika kipindi cha miaka mitano kabla ya Uchaguzi Mkuu awe hajawahi kutiwa hatiani katika Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali.

### 2.2. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

(i) Awe amedhaminiwa na wapiga kura wasiopungua mia mbili (200) waliojiandikisha kupiga kura katika kila mkoa kwa mikoa kumi na kati ya hiyo angalau mikoa

miwili iwe ya Tanzania Zanzibar. **Hii ina maanisha mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais anatakiwa kudhaminiwa na jumla ya wapiga kura wasiopungua 2000 kutoka mikoa 10.**

(ii) Awe ameweka dhamana ya Shilingi Milioni moja (1,000,000/=) Tume kupitia akaunti ya amana atakayopatiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi siku ya kuchukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipia atawasilisha ***pay-in slip*** ya benki kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi ili apatiwe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

(iii) Awe ametoa tamko mbele ya Jaji kwamba anazo sifa zinazotakiwa na hajapoteza sifa hizo.

**2.3. Masharti ya Urejeshaji wa Dhamana za Wagombea**

Mgombea wa kiti cha Rais atarejeshewa dhamana aliyotoa ikiwa atakidhi masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Maelekezo ya Tume. Dhamana za wagombea hurejeshwa baada ya kukamilika kwa zoezi la uchaguzi husika kwa utaratibu ufuatao:-

(i) Endapo mgombea atakuwa amepata moja ya kumi (1/10) au zaidi ya kura zote halali zilizohesabiwa.

(ii) Endapo mgombea amefariki kabla ya Siku ya Uchaguzi, dhamana hiyo itarejeshwa kwa msimamizi wa mirathi anayetambulika kisheria.

Dhamana hiyo itakuwa mali ya Serikali ikiwa: -

(a) Mgombea atajitoa baada ya siku ya uteuzi; au

(b) Kura alizopata mgombea katika uchaguzi ni pungufu ya moja ya kumi (1/10) ya kura zote halali zilizohesabiwa.

### 2.4. Fomu za Uteuzi (Fomu Na. 8A)

Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatoa fomu za uteuzi kwa mgombea aliyetambulishwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu.

Fomu ya uteuzi ya mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais (Fomu Na. 8A) itaonesha: -

(i) Maelezo binafsi ya anayeomba kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Tamko la mgombea kuwa anazo sifa za kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(iii) Uthibitisho wa Katibu Mkuu wa chama cha siasa kumpendekeza mgombea;

(iv) Wapiga kura wanaowadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(v) Tamko la kisheria la mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vi) Uthibitisho kwamba mgombea ameweka dhamana ya shilingi milioni moja (1,000,000/=); na

(vii) Uthibitisho wa Tume wa kumteua mgombea.

### 2.5. Wadhamini wa Wagombea

Watakaowadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais ni wale ambao:-

(i) Wamejiandikisha kuwa wapiga kura katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika mikoa husika;

(ii) Hawajamdhamini mgombea mwingine yeyote wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais; na

(iii) Wamewadhamini wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais kwa kutumia fomu ya uteuzi.

**Angalizo:**

Wadhamini wa wagombea si lazima wawe wanachama wa chama kilichompendekeza mgombea na wala si lazima wawe wanachama wa chama chochote cha siasa.

### 2.6. Uthibitisho wa Msimamizi wa Uchaguzi Juu ya Wadhamini

Wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais watapaswa kuwasilisha fomu za uteuzi kwa Wasimamizi wa Uchaguzi wa jimbo ambalo wadhamini wametoka. Wasimamizi wa Uchaguzi watatakiwa kutoa uthibitisho wa wadhamini hao kwa kujaza sehemu husika katika Fomu Na. 8A kwa kuweka jina kamili, saini na muhuri wa Msimamizi wa Uchaguzi wa jimbo husika.

### 2.7. Uwasilishaji Rasmi wa Fomu za Uteuzi

(i) Wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais watawasilisha rasmi Tume nakala nne (4) za fomu za Uteuzi. Tume ikisha pokea fomu za uteuzi na kujiridhisha kuwa wagombea wanazo sifa za kugombea itawateua.

(ii) Wagombea watawasilisha picha nne za rangi zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria (passport size) zilizopigwa ndani ya miezi

mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (white background) na nyuma ya picha liandikwe jina kamili la mgombea na chama chake.

(iii) Wagombea watawasilisha stakabadhi ya mapokezi ya dhamana ya kiasi cha shilingi milioni moja (1,000,000/=) za kitanzania kutoka Tume.

(iv) Baada ya kuwasilisha fomu ya uteuzi, wagombea watatakiwa kutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi mbele ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kutumia Fomu Na. 10.

(v) Mgombea akitaka anaweza kuwasilisha fomu zake Tume kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi kwa ajili ya ukaguzi na pale ambapo pana dosari mgombea ataelekezwa kurekebisha dosari hizo. Mgombea ahakikishe anarudishiwa fomu zake mara baada ya kukaguliwa. Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume, siku ambayo Tume itapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

**Angalizo:**

1. Ni muhimu siku ya uteuzi mgombea kuwasilisha mwenyewe fomu za uteuzi ili atoe tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi mbele ya Tume.

2. Aidha, ni vema fomu hizo zikawasilishwa mapema ili kuwe na muda wa kutosha wa kuzishughulikia na kama kuna kasoro zinazoweza kurekebishwa kabla ya muda wa uteuzi ziweze kurekebishwa.

## 2.8. Uthibitisho wa Tume Kuwateua Wagombea

Tume baada ya kupokea fomu za uteuzi za wagombea itafanya yafuatayo:-

**(i) Ukaguzi wa Fomu**

Tume itakagua fomu za uteuzi za wagombea wa kiti cha Rais ili kujiridhisha kama imejazwa kikamilifu. Pia, itahakikisha kwamba nyuma ya picha kumeandikwa jina kamili la mgombea na chama chake. Ikiwa mgombea hakuandika jina na chama chake, Tume itamtaka aandike taarifa hizo kabla ya kuondoka. Jambo hilo ni muhimu sana ili kuhakikisha kuwa kwenye karatasi ya kura picha ya mgombea "X" isipewe jina la mgombea "Y".

**(ii) Uteuzi wa Mgombea**

Tume itamteua mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais baada ya kujiridhisha kuwa ametimiza masharti yanayotakiwa.

**(iii) Kubandika Fomu za Uteuzi**

Tume itabandika nakala moja ya Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8A) yenye picha za wagombea, stakabadhi ya malipo na Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi (Fomu Na. 10) kwa wagombea walioteuliwa si zaidi ya saa kumi (10:00) jioni siku ya uteuzi ili ziweze kukaguliwa na iwapo kuna pingamizi liwasilishwe Tume kupitia Fomu Na. 9A.

## 2.9. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Kiti cha Rais na Makamu wa Rais

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais aliyeteuliwa na Tume kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria.

### (i) Wanaoruhusiwa Kuweka Pingamizi

Kwa mujibu kanuni ya 39 ya kanuni ya Uchaguzi wa Rais na Ubunge za mwaka 2020, wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ni wafuatao: -

(a) Mgombea yeyote wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(c) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(d) Msajili wa Vyama vya Siasa.

Viongozi wa vyama vya siasa vilivyowapendekeza wagombea au mtu mwingine yeyote hawana haki kisheria ya kuweka pingamizi.

### (ii) Muda wa Kuweka Pingamizi

Kwa mujibu wa kanuni ya 39 (3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, muda wa kuweka pingamizi ni kuanzia saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku ya uteuzi mpaka saa 10:00 jioni ya siku inayofuata baada ya siku ya uteuzi. Pingamizi zitawekwa kwa kujaza Fomu Na. 9A.

**Msajili wa Vyama vya Siasa anaruhusiwa kuweka pingamizi kuhusu masuala yanayohusu gharama za uchaguzi si chini ya siku saba (7) na si zaidi ya siku 14 baada ya siku ya uteuzi.**

**(iii) Sababu za Pingamizi**

Sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba mgombea:-

(a) Si raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;

(b) Hajatimiza umri wa miaka arobaini;

(c) Hana sifa za kuwa mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(d) Hana sifa za kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi;

(e) Si mwanachama wa chama cha siasa chenye usajili wa kudumu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa;

(f) Hakudhaminiwa na chama cha siasa kugombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais;

(g) Ametiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano (5) kabla ya uchaguzi;

(h) Hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika mikoa 10 ya Jamhuri ya Muungano, ikiwemo angalau mikoa 2 ya Tanzania Zanzibar;

(i) Hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa;

(j) Hakulipa dhamana ya shilingi milioni moja (1,000,000/=) za kitanzania;

(k) Hajaambatisha picha kwenye fomu za uteuzi;

(l) Hakutoa tamko la kisheria kwa mujibu wa kifungu cha 38 (4)(a) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343;

(m) Hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia katika uchaguzi chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu);**

(n) Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria;

(o) Hajatoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020; na

(p) Ametenda vitendo vilivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama Vya Siasa tu**).

Pingamizi lolote ni lazima liwekwe kwa maandishi kwa kutumia Fomu Na. 9A, na lazima litiwe saini na anayeweka pingamizi.

**2.10. Uamuzi wa Tume**

Baada ya kupokea pingamizi, Tume itamjulisha kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi na kumtaka atoe maelezo yake. Baada ya kupokea maelezo, Tume itatoa uamuzi wa kukubali au kukataa pingamizi husika na itawataarifu wahusika uamuzi kuhusu pingamizi hilo.

**Uamuzi wa Tume kuhusu pingamizi dhidi ya mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais utakuwa wa mwisho.**

### 2.11. Kutokuwepo au Kufariki kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 35A cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, ikiwa baada ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi hakuna mgombea aliyeteuliwa kwa kiti cha Rais na Makamu wa Rais au katika muda wowote baada ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi na kabla matokeo ya uchaguzi hayajatangazwa mgombea yeyote wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais atafariki, Tume itatangaza tarehe nyingine ya uteuzi kwa mujibu wa sheria.

### 2.12. Mgombea Pekee wa Kiti cha Rais

Kwa mujibu wa kifungu 34 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura 343 iwapo mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais aliyeteuliwa ni mmoja: -

(i) Tume itatangaza kuwa kuna mgombea pekee wa kiti cha Rais.

(ii) Tume itawasilisha jina lake kwa wananchi kwa ajili ya kupigiwa kura na itachukuliwa kuwa amechaguliwa endapo atapata zaidi ya asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa.

(iii) Endapo mgombea huyo atashindwa kupata zaidi ya asilimia 50, Tume itapanga tarehe nyingine kwa ajili ya Uchaguzi wa Rais.

### 2.13. Kujitoa kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 35 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, mgombea wa kiti cha Rais

anaweza kujitoa kugombea kwa kuwasilisha Tume yeye mwenyewe barua ya kujitoa.

Endapo mgombea atajitoa baada ya muda uliowekwa kisheria atapoteza dhamana ya fedha alizoweka kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi.

## SURA YA TATU

## UTEUZI WA MGOMBEA UBUNGE

### 3.1. Sifa za Mgombea Ubunge

Kwa mujibu wa ibara ya 67 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, mtu yeyote atakuwa na sifa za kustahili kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge endapo: -

(i) Ni raia wa Jamhuri ya Muungano;

(ii) Ametimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(iii) Anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(iv) Ni mwanachama na ni mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa; na

(v) Hajawahi kutiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

### 3.2. Kukosa Sifa za Kugombea Ubunge

Kwa mujibu wa ibara ya 67 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, mtu hataruhusiwa kugombea Ubunge ikiwa: -

(i) Ni raia wa nchi nyingine;

(ii) Kwa mujibu wa Sheria inayotumika katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imethibitishwa rasmi kwamba mtu huyo ana ugonjwa wa akili;

(iii) Amehukumiwa na Mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa gerezani kwa muda unaozidi miezi sita kwa kukutwa na hatia ya kosa lolote, vyovyote linavyoitwa, linaloambatana na utovu wa uaminifu;

(iv) Katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu amepata kuhukumiwa na kupewa adhabu ya kifungo kwa kosa linaloambatana na utovu wa uaminifu au kwa kuvunja Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(v) Si mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;

(vi) Mtu huyo ana maslahi yoyote katika mkataba wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wa aina yoyote aliyowekewa miiko maalum kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge, na iwapo amekiuka miiko hiyo;

(vii) Ameshika madaraka ya Afisa Mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa madaraka ambayo Rais aweza au anatakiwa kukabidhi kwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano au Sheria iliyotungwa na Bunge;

(viii) Kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote, mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kuwa mpiga kura au kupiga kura katika uchaguzi wa Wabunge; na

(ix) Ni mgombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Angalizo:**

1. Mtu aliyepewa adhabu ya kulipa faini au kifungo na akalipa faini hazuiwi kugombea Ubunge. Iwapo atapewa adhabu ya kulipa faini akashindwa na akatumikia kifungo na kukimaliza kabla ya siku ya uteuzi anaruhusiwa kugombea. Hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 67 (7)(a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977.
2. Kiongozi wa chama cha siasa haruhusiwi kupendekeza jina lake na kujidhamini mwenyewe.

### 3.3. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge

Masharti ya uteuzi wa Wagombea Ubunge ni kama ifuatavyo: -

(i) Adhaminiwe na wapiga kura wasiopungua ishirini na tano (25) walioandikishwa kuwa wapiga kura katika jimbo linalohusika. Mgombea haruhusiwi kujidhamini yeye mwenyewe. Mpiga kura anatakiwa kudhamini mgombea Ubunge mmoja tu.

(ii) Awe ametoa tamko mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa zinazotakiwa kugombea Ubunge na hajapoteza sifa hizo.

(iii) Aweke dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa Msimamizi wa Uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku akichukua fomu za

uteuzi. Mgombea akishalipa atawasilisha ***pay - in slip*** ya benki kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apewe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

> **Angalizo:**
>
> Wagombea wahakikishe wanapewa akaunti namba ya amana ya halmashauri kwa ajili ya malipo ya dhamana wanapochukua fomu za uteuzi.

**3.4. Masharti ya Urejeshaji wa Dhamana za Wagombea**

Mgombea atarejeshewa dhamana aliyotoa ikiwa atakidhi masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria na Maelekezo ya Tume. Dhamana za wagombea hurejeshwa baada ya kukamilika kwa zoezi la uchaguzi husika kwa utaratibu ufuataoo:-

(i) Endapo mgombea atakuwa amepata moja ya kumi (1/10) au zaidi ya kura zote halali zilizohesabiwa.

(ii) Endapo mgombea amefariki kabla ya Siku ya Uchaguzi, dhamana hiyo itarejeshwa kwa msimamizi wa mirathi anayetambulika kisheria.

Dhamana hiyo itakuwa mali ya Serikali ikiwa: -

(a) Mgombea atajitoa baada ya siku ya uteuzi; au

(b) Kura alizopata mgombea katika uchaguzi ni pungufu ya moja ya kumi (1/10) ya kura zote halali zilizohesabiwa.

**3.5. Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8B)**

Kwa mujibu wa kifungu cha 38 (3) na (4) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 fomu ya uteuzi wa mgombea Ubunge inajumuisha mambo yafuatayo:-

(i) Maelezo binafsi ya mgombea Ubunge;

(ii) Tamko la mgombea Ubunge kwamba anazo sifa za kugombea;

(iii) Uthibitisho wa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo wa kumteua mgombea;

(iv) Wapiga kura wanaomdhamini mgombea Ubunge;

(v) Tamko la kisheria la mgombea Ubunge;

(vi) Uthibitisho kwamba mgombea ameweka dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=); na

(vii) Uthibitisho wa Msimamizi wa Uchaguzi wa kumteua mgombea.

**3.6. Utoaji wa Fomu za Uteuzi**

Fomu za uteuzi zitatolewa na Wasimamizi wa Uchaguzi kwa wagombea ambao wana ushahidi wa maandishi kutoka kwa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya mkoa, wilaya au jimbo kwamba wamependekezwa na vyama vyao kugombea.

Kila mgombea mwenye ushahidi huo atapewa nakala nne (4) za Fomu za Uteuzi Na. 8B na Fomu Na. 10 ya Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020.

Mgombea akishapatiwa fomu atafanya yafuatayo: -

(i) Atatafuta wapiga kura wasiopungua ishirini na tano (25) watakaokuwa wadhamini wake kwa kumjazia fomu ya uteuzi. Wadhamini hao: -

(a) Wawe wamejiandikisha kuwa wapiga kura katika Jimbo analogombea;

(b) Wawe hawajamdhamini mgombea Ubunge mwingine yeyote; na

(c) Si lazima wawe wanachama wa chama kilichompendekeza, wala si lazima wawe wanachama wa chama chochote cha siasa.

(ii) Atajaza taarifa zake binafsi katika Fomu Na. 8B, na ahakikishe kwamba taarifa hizo zinathibitishwa na chama kilichomteua ngazi mkoa, wilaya au jimbo kwamba ni za kweli. Ni muhimu kuhakikisha kuwa taarifa zilizojazwa katika nakala zote za fomu za uteuzi zinafanana;

(iii) Atatoa tamko mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa za kugombea Ubunge katika nakala zote nne za fomu ya uteuzi;

(iv) Atawasilisha picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria (passport size) zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (white background) na nyuma ya picha hizo liandikwe jina kamili la mgombea, jimbo na chama. Picha hizo ndizo zitakazotumika katika karatasi ya kura; na

(v) Ataweka dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa Msimamizi wa Uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku akichukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipa atawasilisha ***pay -in slip*** ya benki kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apewe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

**Angalizo**:

Fomu za uteuzi zitatolewa kwa mgombea mmoja tu aliyependekezwa na kutambulishwa kwa barua kutoka katika kila chama cha siasa.

**3.7. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi**

Mgombea awasilishe nakala nne (4) za fomu ya uteuzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi. Fomu hizo ziwasilishwe pamoja na: -

(i) Picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria (*passport size*) zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (*white background*) na nyuma ya picha hizo liandikwe jina kamili la mgombea, jimbo na chama.

(ii) Stakabadhi ya malipo ya dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=).

(iii) Fomu Na. 10 ya tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi.

Ni muhimu wagombea kuwasilisha fomu za uteuzi wao wenyewe ili watimize sharti la kutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi. Aidha, ni vema kuwasilisha fomu hizo mapema siku ya uteuzi ili upatikane muda wa kutosha wa kuzishughulikia.

Mgombea akitaka anaweza kuwasilisha fomu zake kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi ili Msimamizi wa Uchaguzi aweze kuzikagua na pale ambapo pana dosari aelekezwe akarekebishe dosari hizo. **Mgombea ahakikishe**

**anarudishiwa fomu zake mara baada ya kukaguliwa.** Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume ambapo Msimamizi wa Uchaguzi atapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

### 3.8. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Ubunge Zaidi ya Mmoja

Kifungu cha 38 (9) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 kinakataza mpiga kura kudhamini zaidi ya mgombea mmoja katika uchaguzi husika.

Kifungu cha 38 (10) cha Sheria tajwa kinaeleza kuwa endapo mpiga kura atadhamini mgombea zaidi ya mmoja na wagombea hao wakateuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi, udhamini huo hautabatilisha uteuzi wao, isipokuwa itakuwa ni kosa kwa mpiga kura huyo kwa mujibu wa kifungu cha 38 (11) cha sheria husika.

Utaratibu wa kushughulikia mpiga kura aliyemdhamini mgombea zaidi ya mmoja ni ufuatao: -

(i) Kwa mujibu wa kifungu cha 38 (11) na (12) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, mpiga kura aliyedhamini mgombea zaidi ya mmoja akikubali kosa kwa maandishi, Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kutoa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki mbili (200,000/=);

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa atoe stakabadhi ya malipo baada ya mdhamini kulipa fedha hizo; na

(iii) Mpiga kura asipokubali kosa kwa maandishi shauri hili litapelekwa Mahakamani.

### 3.9. Kubandika Fomu za Uteuzi wa Wagombea Ubunge

Kwa mujibu wa kifungu cha 38 (8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kanuni ya 29 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, Msimamizi

wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi anatakiwa kubandika nakala moja ya Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8B) yenye picha ya mgombea, stakabadhi ya malipo na Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi (Fomu Na. 10) kwa kila mgombea aliyemteua.

**Fomu hizo na stakabadhi zitabandikwa mahali pa wazi penye usalama nje ya ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi au kabla ya muda huo hadi saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku inayofuata**.

## 3.10. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Ubunge

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea ubunge aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria. Pingamizi linaweza kuwekwa kuanzia saa 10:00 jioni siku ya uteuzi hadi saa 10:00 jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

### (i) Sababu za Pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba Mgombea:-

(a) Si raia wa Tanzania;

(b) Hajatimiza umri wa miaka 21;

(c) Hana sifa za kuwa mgombea Ubunge;

(d) Hawezi kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(e) Si mwanachama wa chama cha siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya

Vyama vya Siasa;

(f) Hakudhaminiwa na chama cha siasa kugombea Ubunge;

(g) Ametiwa hatiani kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi;

(h) Hakudhaminiwa na idadi ya wapiga kura inayotakiwa;

(i) Hakulipa dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=);

(j) Hajaambatisha picha katika fomu ya uteuzi;

(k) Hakuwasilisha tamko la kisheria;

(l) Hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia katika uchaguzi chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278. (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu**);

(m) Hajatoa Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020;

(n) Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na sheria;

(o) Ametenda vitendo vilivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu**); na

(p) Hakudhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika jimbo husika.

**(ii) Wanaoruhusiwa Kuweka Pingamizi**

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 wanaoruhusiwa kuweka pingamizi ni:-

(a) Mgombea Ubunge yeyote wa jimbo linalohusika;

(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(c) Msimamizi wa Uchaguzi;

(d) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na

(e) Msajili wa Vyama vya Siasa.

**(iii) Utaratibu wa Kuweka Pingamizi Dhidi ya Mgombea Ubunge**

Pingamizi lazima liwekwe kwa maandishi kwa kutumia Fomu Na. 9B ikionesha yafuatayo: -

(a) Maelezo ya anayeweka pingamizi;

(b) Jina la mgombea aliyewekewa pingamizi;

(c) Sababu ya pingamizi;

(d) Tarehe na muda wa kuwasilisha pingamizi; na

(e) Saini ya anayeweka pingamizi.

Mgombea, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Uchaguzi watawasilisha fomu ya pingamizi kwa Msimamizi wa Uchaguzi si zaidi ya saa 10:00 jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

**(iv) Utaratibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea**

Msajili wa Vyama vya Siasa atawasilisha pingamizi kwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa kutumia Fomu Na. 9B si chini ya siku saba na si zaidi ya siku 14 baada ya siku ya uteuzi.

Utaratibu wa kushughulikia pingamizi zitakazowekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa dhidi ya mgombea utafuata utaratibu ulioelekezwa katika kipengele **3.12.**

**(v) Utaratibu wa Kushughulikia Pingamizi**

Msimamizi wa Uchaguzi mara baada ya kupokea pingamizi, atatakiwa amtaarifu kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi juu ya pingamizi hilo na kumtaka atoe maelezo yake. Mgombea aliyewekewa pingamizi anaweza kutoa maelezo na kumpa Msimamizi wa Uchaguzi.

Baada ya kupata maelezo ya pande zote zinazohusika, hata kama aliyewekewa pingamizi hatatoa maelezo yake, Msimamizi wa Uchaguzi ataamua haraka iwezekanavyo kama analikubali au analikataa pingamizi hilo. Aliyeweka pingamizi na mgombea aliyewekewa pingamizi watafahamishwa kwa maandishi kuhusu uamuzi na sababu za uamuzi huo.

**Angalizo:**

Viongozi wa vyama vya siasa vilivyowapendekeza wagombea au mtu mwingine yeyote hawana haki kisheria ya kuweka pingamizi.

## 3.11. Utaratibu wa Msimamizi wa Uchaguzi kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (5) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, pale ambapo Msimamizi wa Uchaguzi yeye mwenyewe anaweka pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea, anapaswa kabla ya kuanza kufanya uchunguzi juu

ya pingamizi hilo amtaarifu mgombea anayehusika kwa maandishi. Msimamizi wa Uchaguzi baada ya kukamilisha uchunguzi atawasilisha matokeo ya uchunguzi huo Tume.

### 3.12. Utaratibu wa Kukata Rufaa

Kifungu cha 40 (6) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, kinaruhusu wagombea kukata rufaa Tume kupinga uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi dhidi yao.

Kwa utekelezaji bora wa suala hili, Tume imeweka masharti yafuatayo:-

(i) Rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu uteuzi wa mgombea Ubunge zitawasilishwa kwa kujaza Fomu Na. 12. Warufani watajaza nakala tatu (3) za fomu hizo ambazo watazipata kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

(ii) Kwa mujibu wa kanuni ya 31 (1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020, fomu ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika muda wa saa ishirini na nne (24) tangu Msimamizi wa Uchaguzi alipotoa uamuzi unaopingwa. Msimamizi wa Uchaguzi atapokea rufaa hizo kwa niaba ya Tume na ataandika muda wa kupokea, ataweka saini na kugonga muhuri wa Msimamizi wa Uchaguzi.

### 3.13. Uamuzi wa Tume

Tume, wakati wa kushughulikia rufaa ya mgombea Ubunge inaweza kumwita mtu yeyote kutoa ushahidi au maelezo ya ziada au ufafanuzi kuhusiana na rufaa husika. Uamuzi wa Tume kuhusu rufaa utakuwa ni wa mwisho na ambaye

hajaridhika nao, anaweza baada ya uchaguzi, kuwasilisha malalamiko yake Mahakama Kuu.

**3.14. Kutokuwepo kwa Wagombea**

Kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 endapo baada ya uteuzi hapatakuwa na mgombea yeyote kwa sababu ya kifo, kujitoa, au sababu nyingine yoyote kama vile kutojitokeza kwa wagombea, Msimamizi wa Uchaguzi aitaarifu Tume ili iweze kusitisha uchaguzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea katika jimbo husika kwa mujibu wa sheria.

**3.15. Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa**

Kwa mujibu wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, endapo mgombea aliyeteuliwa ni mmoja atahesabika kuwa amechaguliwa na upigaji kura hautafanyika katika jimbo hilo kwa uchaguzi wa Mbunge. Aidha, Msimamizi wa Uchaguzi atamtaarifu kwa barua mgombea aliyechaguliwa baada ya muda wa pingamizi kupita. Mgombea husika atapatiwa hati ya kuchaguliwa kuwa Mbunge mara baada ya uchaguzi kukamilika.

**3.16. Kujitoa kwa Mgombea**

Kwa mujibu wa kifungu cha 48 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, mgombea anaweza kujitoa kugombea kwa kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi yeye mwenyewe barua ya kujitoa pamoja na tamko la kujitoa alilotoa mbele ya Hakimu. Nakala ya barua ya kujitoa ipelekwe tawi la chama kilichomdhamini kabla ya saa kumi na mbili (12:00) jioni, siku inayofuata baada ya siku ya uteuzi.

Endapo mgombea atajitoa baada ya muda uliowekwa kisheria atapoteza dhamana ya fedha alizoweka kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

Kwa mujibu wa kanuni ya 34 (2) (b) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 mgombea akijitoa baada ya siku ya uteuzi, chama chake hakitapata nafasi ya kuweka mgombea mwingine.

**3.17. Kufariki kwa Mgombea**

Kwa mujibu wa kifungu cha 49 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, endapo Msimamizi wa Uchaguzi atajiridhisha kuwa mgombea yeyote amefariki baada ya saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku ya uteuzi na kabla ya muda wa mwisho wa upigaji kura, atasitisha uchaguzi katika jimbo husika na kutoa taarifa Tume ili ipange tarehe nyingine ya uteuzi wa mgombea wa chama ambacho mgombea wake amefariki.

# SURA YA NNE

# UTEUZI WA WAGOMBEA UDIWANI

## 4.1. Sifa za Mgombea Udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 39 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 sifa za mgombea Udiwani ni zifuatazo:-

(i) Awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Awe ametimiza umri wa miaka ishirini na moja (21);

(iii) Awe anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(iv) Awe mkazi wa kawaida wa halmashauri anayogombea;

(v) Awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa chenye usajili wa kudumu;

(vi) Awe na kipato halali kinachomwezesha kuishi; na

(vii) Awe hajatiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi.

## 4.2. Kukosa Sifa za Kugombea Udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 mtu hataruhusiwa kugombea Udiwani ikiwa:-

(i) Ana utii wa nchi nyingine;

(ii) Amethibitika kisheria kwamba hana akili timamu;

(iii) Amehukumiwa kifo na Mahakama Kuu au Mahakama ya Rufaa Tanzania;

(iv) Anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita gerezani kilichotolewa na Mahakama yoyote Tanzania;

(v) Yuko uhamishoni kwa zaidi ya miezi sita kwa mujibu wa Sheria ya Uhamishoni (*Deportation Act, Cap 380*);

(vi) Amezuiwa na Sheria yoyote nchini kujiandikisha kuwa mpiga kura; na

(vii) Ana maslahi katika mkataba na halmashauri au kampuni yenye mkataba na halmashauri na hajatangaza kwenye magazeti yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza yanayopatikana katika halmashauri husika juu ya maslahi hayo.

**Angalizo:**

Kwa mujibu wa kifungu cha 40 (2) (b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 mtu aliyepewa adhabu ya kulipa faini au kifungo na akalipa faini hazuiwi kugombea Udiwani. Iwapo atapewa adhabu ya kulipa faini akashindwa na akatumikia kifungo na kukimaliza kabla ya siku ya uteuzi anaruhusiwa kugombea.

Kiongozi wa chama cha siasa haruhusiwi kupendekeza jina lake na kujidhamini mwenyewe.

### 4.3. Masharti ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ili mgombea Udiwani aweze kuteuliwa anapaswa atimize masharti yafuatayo: -

(i) Awe amedhaminiwa na wapiga kura wasiopungua kumi (10) walioandikishwa katika kata anayogombea.

(ii) Awe ametoa Tamko mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa za kugombea Udiwani na hajapoteza sifa hizo.

(iii) Awe ameweka dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=) kwa Msimamizi wa Uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku ya kuchukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipa atawasilisha ***pay - in slip*** ya benki kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apewe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

**Angalizo**: Wagombea wahakikishe wanapewa akaunti namba ya amana ya halmashauri kwa ajili ya malipo ya dhamana wanapochukua fomu za uteuzi.

### 4.4. Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8C)

Kwa mujibu wa kifungu cha 42 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 fomu ya uteuzi ya mgombea Udiwani itaonesha: -

(i) Maelezo binafsi ya mgombea;

(ii) Tamko la mgombea Udiwani kwamba anazo sifa za kugombea;

(iii) Uthibitisho wa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya wilaya, jimbo au kata wa kumpendekeza kuwa mgombea;

(iv) Tamko, majina, anuani na namba za wapiga kura wasiopungua kumi waliomdhamini mgombea;

(v) Tamko la kisheria la mgombea kuthibitisha kwamba anazo sifa zinazotakiwa kugombea Udiwani na hajapoteza sifa hizo;

(vi) Uthibitisho kuwa mgombea ameweka dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=); na

(vii) Uthibitisho wa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kumteua mgombea.

**4.5. Utoaji wa Fomu za Uteuzi**

(i) Fomu za uteuzi zitatolewa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi kata kwa mgombea ambaye ana ushahidi wa maandishi kutoka kwa Katibu wa chama cha siasa ngazi ya wilaya, jimbo au kata kwamba amependekezwa na chama chake.

(ii) Kila mgombea mwenye ushahidi huo atapewa nakala nne (4) za Fomu za Uteuzi (Fomu Na. 8C) na Fomu za Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 (Fomu Na. 10). Fomu hizo zitatolewa kwa mgombea mmoja tu aliyependekezwa kutoka kila chama cha siasa.

(iii) Mgombea akishapatiwa fomu atafanya yafuatayo: -

(a) Apate wapiga kura wasiopungua kumi (10) watakaokuwa wadhamini wake kwa kumjazia fomu ya uteuzi. Wadhamini hao:-

(i) Wawe wamejiandikisha kuwa wapiga kura katika kata anayogombea;

(ii) Wawe hawajamdhamini mgombea Udiwani mwingine yeyote; na

(iii) Si lazima wawe wanachama wa chama kilichompendekeza au wanachama wa chama chochote cha siasa.

(b) Ajaze taarifa zake binafsi kwenye Fomu Na. 8C, na ahakikishe kwamba taarifa hizo zinathibitishwa na Katibu wa chama kilichomteua ngazi wilaya, jimbo au kata kwamba ni za kweli. Ni muhimu ahakikishe kuwa taarifa zilizojazwa katika nakala zote nne za fomu zinafanana.

(c) Atoe tamko mbele ya Hakimu kuthibitisha kwamba anazo sifa za kugombea Udiwani katika nakala zote nne za fomu ya uteuzi.

(d) Awe na picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha zinazotumika kwenye pasi ya kusafiria (passport size) zilizopigwa ndani ya miezi mitatu kabla ya siku ya uteuzi. Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (white background) na nyuma liandikwe jina kamili la mgombea, kata na chama. Picha hizo ndizo zitakazotumika katika karatasi ya kura; na

(e) Aweke dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=) kwa Msimamizi wa Uchaguzi kupitia akaunti ya amana ya halmashauri atakayopatiwa siku ya kuchukua fomu za uteuzi. Mgombea akishalipia atawasilisha pay***-in slip*** ya benki kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apewe stakabadhi ya kukiri mapokezi.

**4.6. Uwasilishaji wa Fomu Siku ya Uteuzi**

Mgombea anayependekezwa na chama cha siasa awasilishe kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kabla ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya uteuzi nyaraka zifuatazo: -

(a) Nakala nne (4) za fomu ya uteuzi;

(b) Picha nne (4) za rangi zenye ukubwa sawa na picha inayotumika katika pasi ya kusafiria (*passport size*). Muonekano wa picha kwa nyuma uwe wa rangi nyeupe (*white background*) na nyuma liandikwe jina kamili la mgombea, kata na chama; na

(c) Stakabadhi ya malipo ya dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=).

Mgombea anaweza kuwasilisha fomu zake kuanzia siku tatu (3) kabla ya siku ya uteuzi ili Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata aweze kuzikagua na ikiwa kuna dosari amuelekeze mgombea akarekebishe dosari hizo. **Mgombea ahakikishe anarudishiwa fomu zake mara baada ya kukaguliwa.** Hata hivyo, uteuzi rasmi utafanywa siku iliyotangazwa na Tume ambapo Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata atapaswa kupokea fomu husika kutoka kwa wagombea na kufanya uteuzi.

Ni muhimu wagombea wawasilishe fomu za uteuzi wao wenyewe ili watimize sharti la kutoa tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi. Aidha, ni vema kuwasilisha fomu hizo mapema siku ya uteuzi ili upatikane muda wa kutosha wa kuzishughulikia.

### 4.7. Mpiga Kura Anayedhamini Mgombea Udiwani Zaidi ya Mmoja

Kifungu cha 42 (9) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kinakataza mpiga kura kudhamini zaidi ya mgombea mmoja katika uchaguzi unaohusika.

Kifungu cha 42 (10) cha Sheria tajwa kinaeleza kuwa endapo mpiga kura atadhamini mgombea zaidi ya mmoja na wagombea hao wakateuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi, udhamini huo hautabatilisha uteuzi wao, isipokuwa itakuwa ni kosa kwa mpiga kura huyo kwa mujibu wa kifungu cha 42 (11) cha sheria husika.

Utaratibu wa kushughulikia mpiga kura aliyemdhamini mgombea zaidi ya mmoja ni ufuatao:-

(i) Kwa mujibu wa kifungu cha 42 (11) na (12) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mpiga kura aliyedhamini mgombea zaidi ya mmoja akikubali kosa kwa maandishi, Msimamizi wa Uchaguzi anaweza kutoa adhabu ya faini isiyozidi shilingi laki mbili (200,000/=).

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa atoe stakabadhi ya malipo baada ya mdhamini kulipa fedha hizo.

(iii) Mpiga kura asipokubali kosa kwa maandishi shauri hili litapelekwa Mahakamani.

### 4.8. Kubandika Fomu za Uteuzi wa Wagombea Udiwani

Kwa mujibu wa kifungu cha 42 (8) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za mitaa, Sura ya 292 na kanuni ya 27 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata anatakiwa kubandika nakala moja ya Fomu ya Uteuzi (Fomu Na. 8C) yenye picha ya mgombea, stakabadhi ya malipo na Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi (Fomu Na. 10) kwa kila mgombea aliyemteua.

Fomu hizo na stakabadhi zitabandikwa mahali pa wazi nje ya ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata saa kumi kamili (10:00) jioni siku ya

uteuzi au kabla ya muda huo hadi saa kumi kamili (10:00) jioni ya siku inayofuata.

### 4.9. Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani

Pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea linalenga kuweka zuio kwa mgombea Udiwani aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kwamba hana sifa za kuteuliwa kwa mujibu wa sheria. Pingamizi linaweza kuwekwa kuanzia saa 10:00 jioni siku ya uteuzi hadi saa 10:00 jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

#### (i) Sababu za Pingamizi

Kwa mujibu wa kifungu cha 44 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 sababu ya pingamizi inaweza kuwa yoyote kati ya zifuatazo, kwamba Mgombea:-

(a) Si raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) Hajatimiza umri wa miaka 21;

(c) Hajui kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza;

(d) Si mwanachama wa chama cha siasa chenye usajili wa kudumu;

(e) Si mkazi wa kawaida wa halmashauri ambayo kata anayogombea imo;

(f) Ametiwa hatiani na Mahakama yoyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi yoyote

ya Serikali katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi;

(g) Hajadhaminiwa na wapiga kura walioandikishwa katika kata husika,

(h) Hajadhaminiwa na wapiga kura wasiopungua kumi (10);

(i) Hakuna uthibitisho kuwa mgombea ameweka dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=);

(j) Hakuwasilisha picha;

(k) Hajawasilisha Tamko la Kisheria;

(l) Hajadhaminiwa na chama cha siasa kilichosajiliwa;

(m) Hakutaja gharama na vyanzo vya fedha atakazotumia kwenye uchaguzi (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu**);

(n) Hajatoa Tamko la kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020;

(o) Hakurudisha fomu za uteuzi kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Sheria; na

(p) Ametenda vitendo vilivyokatazwa chini ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi, Sura ya 278 (**Pingamizi kuhusiana na sababu hii litawekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa tu**).

**(ii) Wanaoruhusiwa Kuweka Pingamizi**

(a) Mgombea Udiwani yeyote wa kata inayohusika;

(b) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata; na

(c) Msajili wa Vyama vya Siasa

**(iii) Utaratibu wa Kuweka Pingamizi**

Pingamizi ni lazima liwekwe kwa maandishi kwa kutumia Fomu Na. 9C. Fomu hizo zinapaswa kujazwa nakala mbili zikionyesha yafuatayo:-

(a) Maelezo ya anayeweka pingamizi;

(b) Jina la mgombea aliyewekewa pingamizi;

(c) Sababu za pingamizi;

(d) Tarehe na muda wa kuwasilisha pingamizi; na

(e) Saini ya aliyeweka pingamizi.

Mgombea, Msimamizi wa Uchaguzi au Mkurugenzi wa Uchaguzi atawasilisha fomu ya pingamizi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata si zaidi ya saa kumi kamili (10:00) jioni siku inayofuatia baada ya siku ya uteuzi.

**(iv) Utaratibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa Kuweka Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea**

Msajili wa Vyama vya Siasa atawasilisha pingamizi kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kwa kutumia Fomu Na. 9C si chini ya siku saba na si zaidi ya siku 14 baada ya siku ya uteuzi.

Utaratibu wa kushughulikia pingamizi zitakazowekwa na Msajili wa Vyama vya Siasa dhidi ya mgombea utafuata utaratibu ulioelekezwa katika kipengele **(v).**

**(v) Kushughulikia Pingamizi Dhidi ya Uteuzi wa Mgombea Udiwani**

(a) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata mara baada ya kupokea pingamizi atamtaarifu kwa maandishi mgombea aliyewekewa pingamizi kuhusu pingamizi hilo na kumtaka atoe maelezo yake. Mgombea aliyewekewa pingamizi anaweza kutoa maelezo na kumpa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata maelezo yake.

(b) Baada ya kupata maelezo ya pande zote Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atafanya maamuzi haraka iwezekanavyo ikiwa analikubali au analikataa pingamizi husika.

(c) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata baada ya kufanya uamuzi kuhusu pingamizi awasilishe uamuzi huo kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili aupitie na kuona kama umezingatia sheria. Msimamizi wa Uchaguzi ana mamlaka ya kubadili uamuzi huo kama atabaini kuwa haukuzingatia matakwa ya sheria.

(d) Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kutoa maamuzi ya kukubaliana au kukataa uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata, Wagombea watafahamishwa kwa maandishi kuhusu uamuzi huo. Aidha, Msimamizi wa Uchaguzi kama analikubali pingamizi hilo atatakiwa kuwajulisha wagombea sababu za uamuzi wake.

**Angalizo:**

Viongozi wa vyama vya siasa waliowapendekeza wagombea au mtu mwingine yeyote hawana haki kisheria ya kuweka pingamizi.

### 4.10. Utaratibu wa Kuwasilisha Rufaa

Kifungu cha 44 (5) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kinaruhusu wagombea kukata rufaa Tume dhidi ya uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu pingamizi dhidi yao.

Katika utekelezaji bora wa suala hili masharti yafuatayo yatazingatiwa:-

(i) Rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu uteuzi wa mgombea Udiwani zitawasilishwa kwa kutumia Fomu Na. 12. Warufani watajaza nakala tatu (3) za fomu hizo. Fomu hizo zitatolewa na Wasimamizi wa Uchaguzi.

(ii) Fomu za rufaa ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika muda wa saa ishirini na nne (24) tangu Msimamizi wa Uchaguzi alipotoa uamuzi unaopingwa. Msimamizi wa Uchaguzi apokee rufaa hizo kwa niaba ya Tume. Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 29 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020.

(iii) Msimamizi wa Uchaguzi atamueleza yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wake kuwa ana haki ya kukata rufaa Tume, ndani ya muda wa saa ishirini na nne (24) tangu kutolewa kwa uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi.

### 4.11. Uamuzi wa Tume

Uamuzi wa Tume kuhusu rufaa utakuwa ni wa mwisho na ambaye hataridhika nao, anaweza baada ya uchaguzi, kuwasilisha malalamiko ya uchaguzi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi.

### 4.12. Kutokuwepo kwa Wagombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 52 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, endapo baada ya uteuzi hapatakuwa na mgombea yeyote kwa sababu ya kifo, kujitoa au sababu nyingine yoyote Msimamizi wa Uchaguzi ataitaarifu Tume ili iweze kusitisha uchaguzi na kupanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea katika kata husika.

### 4.13. Mgombea Aliyepita Bila Kupingwa

Kwa mujibu wa kifungu cha 45 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, endapo mgombea aliyeteuliwa ni mmoja atahesabika kuwa amechaguliwa na upigaji kura hautafanyika katika kata hiyo kwa uchaguzi wa Diwani. Aidha, Msimamizi wa Uchaguzi atamtangaza mgombea aliyechaguliwa baada ya muda wa pingamizi kupita. Mgombea husika atapatiwa hati ya kuchaguliwa kuwa Diwani mara baada ya uchaguzi kukamilika.

### 4.14. Kujitoa kwa Mgombea

Kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, mgombea anaweza kujitoa kugombea kwa kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi yeye mwenyewe barua ya kujitoa pamoja na tamko la kujitoa alilotoa mbele ya Hakimu. Nakala ya barua ya kujitoa ipelekwe tawi la chama kilichomdhamini kabla ya saa kumi na mbili (12:00) jioni ya siku inayofuata baada ya siku ya uteuzi.

Endapo mgombea atajitoa baada ya muda wa uteuzi kupita atapoteza dhamana ya fedha alizoweka kwa Msimamizi wa Uchaguzi na chama chake hakitapata nafasi ya kuteua mgombea mwingine.

# SURA YA TANO

# UTARATIBU WA WATUMISHI WA UMMA KUGOMBEA UBUNGE NA UDIWANI

## 5.1. Wanaoruhusiwa na Wasioruhusiwa Kugombea Miongoni mwa Watumishi wa Umma

Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2015 unawaruhusu watumishi wote wa Umma watakaopenda kugombea nyadhifa za kisiasa katika ngazi mbalimbali kufanya hivyo, isipokuwa wale ambao kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawaruhusiwi kuwa wanachama wa chama chochote cha siasa wala kujihusisha na shughuli za kisiasa zaidi ya kupiga kura. Watumishi hao ni:-

(i) Askari wote walio kazini, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(ii) Majaji na Mahakimu wa Mahakama katika ngazi zote;

(iii) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe na Watumishi wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Wasimamizi wa Uchaguzi; na

(iv) Vyombo vingine vya utendaji Serikalini ambavyo kwa hulka yake na kwa mujibu wa utendaji wake wa kazi, watumishi wake hawaruhusiwi kuwa wanachama wa chama chochote cha Siasa na/au kushiriki katika

mambo ya Siasa. Hao ni pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Idara ya Usalama wa Taifa, Mawakili wa Serikali na Watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

**5.2. Wakati wa Kujitayarisha Kugombea**

Mtumishi wa Umma atakayeamua kugombea nafasi ya uongozi wa kisiasa atatakiwa kutoa taarifa rasmi kwa maandishi kwa mamlaka iliyomuajiri na kisha ataomba na atapewa likizo bila malipo ili ashughulikie taratibu zake za kugombea nafasi aliyoomba. Utaratibu utakuwa kama ifuatavyo: -

(i) Kwa wagombea Ubunge na wagombea Udiwani, likizo hiyo itaanza tangu siku ya kuvunjwa Bunge na itakoma tarehe ya kuteuliwa na Tume kuwa mgombea.

(ii) Kwa upande wa Viti Maalum vya Ubunge na Udiwani, likizo hiyo itaanza siku ya kuvunjwa Bunge hadi tarehe ambayo Tume itamtangaza kuwa Mbunge au Diwani.

**5.3. Baada ya Kuteuliwa au Kutangazwa na Tume**

Utaratibu kwa watumishi wote wa Umma watakaogombea nyadhifa za kisiasa nchini utakuwa kama ifuatavyo: -

(i) Mtumishi wa Umma atakayeamua kugombea nafasi ya Ubunge anaruhusiwa kufanya hivyo, na baada ya Tume kumtangaza kuwa mgombea wa Ubunge, atalazimika kuacha kazi;

(ii) Mtumishi wa Umma atakayeamua kugombea Ubunge kupitia Viti Maalum, anaruhusiwa kufanya hivyo, na

baada ya Tume kumtangaza kuwa Mbunge, utumishi wake utakoma; na

(iii) Mtumishi wa Umma, atakayeamua kugombea nafasi ya Udiwani anaruhusiwa kufanya hivyo na baada Tume kumtangaza kuwa Mgombea wa Udiwani, atalazimika kuacha kazi.

## SURA YA SITA

## KAMPENI NA MAADILI YA UCHAGUZI

### 6.1. Kipindi cha Kampeni

Kwa mujibu wa kifungu cha 46 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 53 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 kipindi cha kampeni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani hutangazwa na Tume. Kampeni zitaanza siku moja baada ya siku ya uteuzi na kumalizika siku moja kabla ya siku ya uchaguzi.

Kwa kuzingatia kanuni ya 40 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 35 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020 zikisomwa pamoja na kipengele cha 2.1(c) cha Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020, muda wa kuanza kampeni utakuwa saa mbili kamili (2:00) asubuhi na kumalizika saa kumi na mbili kamili (12:00) jioni.

### 6.2. Wajibu wa Vyama vya Siasa, Wagombea na Mawakala

Wakati wa Kampeni vyama vya siasa vinatakiwa kunadi sera na wagombea wao kwa kuzingatia Sheria za Uchaguzi, Kanuni na Maadili ya Uchaguzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 51 (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 53 (1) (b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, jukumu la kuendesha kampeni za uchaguzi ni la mgombea, wakala wa mgombea au chama chake.

Hivyo, kila mgombea au wakala anatakiwa apange ratiba ya mikutano ya kampeni na kuiwasilisha kwenye chama chake

cha siasa ili iwasilishwe Tume, au kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata tayari kwa kuoanishwa na Ratiba nyingine za wagombea au vyama vya siasa au mawakala.

Mapendekezo ya ratiba za mikutano ya kampeni yanatakiwa kuwasilishwa katika mamlaka husika siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi.

Kwa upande wa uchaguzi wa Rais, ratiba za kampeni zitaratibiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi. Hivyo, vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi wa Rais viwasilishe mapendekezo ya ratiba za mikutano ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi. Mapendekezo hayo yaoneshe tarehe, muda, mkoa, wilaya na mahali ambapo mgombea atafanya kampeni zake. Mkurugenzi wa Uchaguzi baada ya kupokea mapendekezo ataitisha mkutano wa wawakilishi wa vyama vinavyoshiriki uchaguzi wa Rais ili kujadili na kupanga ratiba hiyo. Nakala ya ratiba hiyo itapelekwa kwa wafuatao: -

(i) Vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi wa Rais;

(ii) Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa;

(iii) Wakuu wa Mikoa kwa taarifa; na

(iv) Inspekta Jenerali wa Polisi kwa ajili ya kuandaa ulinzi.

Vyama vya siasa vinatakiwa kuzingatia ratiba hiyo kikamilifu. Pamoja na ratiba hiyo, vyama vya siasa vinaruhusiwa kipindi cha kampeni kufanya kampeni za nyumba kwa nyumba hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 51 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu

cha 53 (1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292.

### 6.3. Wajibu wa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Kata katika Kuratibu Ratiba za Kampeni za Wagombea Ubunge na Udiwani

(i) Kwa uchaguzi wa Ubunge na Udiwani, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atapaswa kabla ya kuanza kwa kampeni za uchaguzi, kuvitaka vyama vya siasa kuwasilisha Ratiba za Kampeni zikionesha tarehe, mahali na saa ya kufanya mikutano ya kampeni.

(ii) Kupokea mapendekezo ya ratiba za kampeni kutoka kwenye vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi. Ratiba za kampeni zitaonesha tarehe, muda, na mahali ambapo mgombea atafanya kampeni zake.

(iii) Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kupokea ratiba zote za kampeni za uchaguzi ataitisha mkutano wa vyama vya siasa au wagombea wanaoshiriki uchaguzi kwa ajili ya kuratibu ratiba hizo ili kuepusha mgongano wakati wa kampeni.

(iv) Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kutayarisha ratiba ya kampeni iliyoratibiwa atasambaza nakala kwa wafuatao: -

  (a) Vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi wa Ubunge au Udiwani;

(b) Mkuu wa Wilaya - kwa taarifa;

(c) Kamanda wa Polisi wa Wilaya kwa madhumuni ya kutoa ulinzi katika mikutano ya Kampeni; na

(d) Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Jimbo na Kata.

**Angalizo:**

Ratiba ya Kampeni iliyowasilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kwa Kamanda wa Polisi wa Wilaya ndiyo taarifa rasmi ya mikutano ya kampeni na atatakiwa kutoa Ulinzi katika mikutano kwa vyama vyote vya siasa. Hivyo, vyama havitatakiwa kuomba vibali vyovyote vya ziada kuendesha mikutano ya kampeni.

**6.4. Utaratibu wa Kubadili Ratiba ya Kampeni**

Endapo chama cha siasa kinakusudia kufanya marekebisho ya eneo la kampeni au kubadilisha ratiba, kitamfahamisha kwa maandishi Mkurugenzi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata na kuainisha sababu za kutaka kufanya hivyo.

Mkurugenzi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Uchaguzi ataitisha mkutano wa vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi husika ili kujadili na kukubaliana juu ya mabadiliko hayo na kisha atavipatia nakala ya ratiba yenye mabadiliko husika vyama vyote vinavyoshiriki katika uchaguzi, Mkuu wa Wilaya na Kamanda wa Polisi wa Wilaya.

**6.5. Maelekezo ya Jumla**

(i) Ni marufuku kwa mgombea, chama cha siasa au wakala, kufanya kampeni siku ya uchaguzi.

(ii) Siku ya Uchaguzi, mpiga kura au mtu mwingine yeyote haruhusiwi kwenda katika kituo cha kupigia kura na alama au vazi au bango linaloashiria kukipigia kampeni chama au mgombea.

(iii) Endapo vyama vya siasa au mgombea yeyote atahitaji kutumia machapisho kama vile mabango au vipeperushi vyenye matangazo ya kampeni anapaswa kuomba idhini kwa mamlaka husika kama ifuatavyo:-

(a) Kwa uchaguzi wa kiti cha Rais kibali kiombwe Tume; na

(b) Kwa uchaguzi wa Ubunge au Udiwani kibali kiombwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

(iv) Msimamizi wa Uchaguzi atatoa Mfano wa Karatasi za Kura kwa vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi ili wapate kuzifahamu na kuzitumia katika mikutano ya kampeni. Karatasi hizo zitakuwa na majina, nembo za vyama na picha za wagombea. Aidha, atatoa mfano wa jalada la nukta nundu (*tactile ballot folder*) litakalotumika kuwawezesha wasioona kupiga kura wenyewe ili litumike kuwaelekeza namna watakavyo kitumia katika kupiga kura.

> **Angalizo**:
>
> Mabango ambayo hayajaidhinishwa na mamlaka husika hayataruhusiwa kutumika katika kampeni.

## 6.6. Maadili ya Uchaguzi

Maadili ya Uchaguzi ni makubaliano ya pamoja baina ya vyama vya siasa, Serikali na Tume yanayoeleza mambo yanayotakiwa kufanywa au kuzingatiwa na yasiyotakiwa

kufanywa katika mchakato wa uchaguzi wakati wa kampeni za uchaguzi, kupiga kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Pamoja na mambo mengine, Maadili ya Uchaguzi yanahusu kuheshimiana, kuzingatia ratiba za kampeni, kuelimisha wanachama wa vyama katika misingi ya kuelewa sera za vyama husika, kutojenga chuki, kushirikiana na kutobeba silaha za aina yoyote katika mikutano.

Vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vinatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi au Msimamizi wa Uchaguzi majina ya watu watakaounda kamati za maadili katika ngazi ya taifa, jimbo au kata siku saba (7) kabla ya siku ya uteuzi wa wagombea.

Kamati hizo zitasimamia na kushughulikia malalamiko yanayotokana na ukiukwaji wa maadili wakati wa kampeni za uchaguzi kuanzia hatua ya kuanza kwa kampeni hadi kukamilika kwa kampeni za uchaguzi.

Vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vina wajibu wa kuhakikisha vinatekeleza makubaliano ya kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi ili kuhakikisha kuwa kampeni zinafanyika kwa amani na utulivu.

Ni muhimu vyama vya siasa na wagombea kuzingatia Kanuni za Maadili ya Uchaguzi ya mwaka 2020 kwani kushindwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha kuharibika kwa mchakato wa uchaguzi.

# SURA YA SABA

# UPIGAJI KURA

## 7.1. Vituo vya Kupigia Kura na Uteuzi wa Watendaji wa Vituo

### (i) Orodha ya Vituo vya Kupigia kura

Msimamizi wa Uchaguzi atavipatia vyama vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi orodha ya vituo vya kupigia kura vitakavyotumika siku kumi na nne (14) kabla ya Siku ya Uchaguzi. Vyama vya Siasa vinaweza kutoa maoni kuhusu mahali vilipo vituo hivyo.

### (ii) Watendaji wa Vituo vya Kupigia Kura

Katika kila kituo cha kupigia kura kutakuwa na watendaji wafuatao: -

- Msimamizi wa Kituo;
- Wasimamizi Wasaidizi wa Kituo wawili (2);
- Karani Mwongozaji Wapiga Kura; na
- Mlinzi wa Kituo.

### (iii) Uteuzi wa Wasimamizi wa Vituo

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatangaza kwenye ubao wa matangazo mahali pa wazi nje ya Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi orodha ya majina ya watu anaotarajia kuwateua kuwa Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura.

## 7.2. Haki ya Vyama vya Siasa na Wagombea Kuteua Mawakala

Kwa mujibu wa kifungu cha 57 (1) na (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, na kifungu cha 58 (1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, chama cha siasa kinaruhusiwa baada ya kupata ridhaa ya mgombea au wagombea kuteua na kuwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi orodha ya majina ya mawakala wa upigaji kura siku saba (7) kabla ya siku ya uchaguzi. Ni vema mawakala wapangiwe vituo vya kupigia kura ndani ya kata wanayoishi ili waweze kuwatambua wapiga kura.

Kila chama cha siasa kitakuwa na wakala mmoja tu kwa kituo ambaye atawakilisha wagombea wa chama hicho kwa uchaguzi wa Rais, Mbunge na Diwani katika kituo husika.

## 7.3. Utambulisho wa Mawakala wa Vyama Vya Siasa

Kwa mujibu wa kanuni ya 50 (6) ya Kanuni Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 43 (6) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, barua ya utambulisho wa kila wakala itakayowasilishwa na chama iainishe kituo alichopangiwa na iambatishwe na picha mbili (*passport size*) zilizopigwa si zaidi ya miezi mitatu.

Aidha, kwa mujibu wa kifungu 57 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 chama kitaruhusiwa kuteua wakala mbadala endapo aliyeteuliwa awali amefariki au ameshindwa kutekeleza majukumu ya uwakala. Katika kurahisisha utekelezaji wa suala hili, sambamba na orodha ya mawakala wa vituoni, vyama viwasilishe majina mawili ya mawakala

wa ziada kwa kila kata ambao watatumika kama mawakala mbadala iwapo itahitajika.

Endapo wakala hana picha anaweza kuwasilisha nakala mbili za mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo: -

(i) Kadi ya mpiga kura;

(ii) Kitambulisho cha Taifa;

(iii) Leseni ya udereva; au

(iv) Pasi ya kusafiria.

Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi kupokea utambulisho wa mawakala atafanya yafuatayo: -

(i) Ataandaa orodha ya mawakala kwa kila kituo.

(ii) Ataikabidhi orodha hiyo kwa Wasimamizi wa vituo pamoja na barua ya utambulisho yenye picha wakati wa kugawa vifaa. Kama barua haina picha iambatishwe na moja ya nakala za vitambulisho vilivyotajwa hapo juu.

(iii) Atawaelekeza Wasimamizi wa Vituo kubandika orodha ya mawakala watakayopatiwa nje ya kituo cha kupigia kura kabla ya kuanza kwa zoezi la upigaji kura.

(iv) Atawaelekeza Wasimamizi wa Vituo wasiombe utambulisho mwingine wowote kutoka kwa mawakala wa vyama.

Tume inashauri uteuzi wa mawakala uzingatie uwiano wa kijinsi na makundi maalum kama vile vijana na watu walemavu. Hata hivyo, vyama vya siasa vina mamlaka kamili juu ya uamuzi wa kuteua mawakala kwa kadri watakavyoona inafaa.

**Angalizo:**

1. Nakala ya fomu ya kiapo (Fomu Na. 6) haitatumika kwa ajili ya utambulisho wa wakala na wakala hatapewa nakala ya fomu hiyo baada ya kuapa.
2. Gharama za mawakala wa vyama vya siasa zitalipwa na vyama vyao.

### 7.4. Kiapo cha Kutunza Siri kwa Mawakala

Kwa mujibu wa kanuni ya 50 (4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge ya mwaka 2020 na kanuni ya 43 (4) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, mawakala wa upigaji kura wanatakiwa kuapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi siku saba (7) kabla ya Siku ya Uchaguzi kwa kutumia Fomu Na. 6.

Wakala ambaye hajaapa hataruhusiwa kuingia kwenye kituo cha kupigia kura.

Kwa mujibu wa kifungu cha 93 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 92 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, endapo mgombea atahitaji kuingia kwenye vituo vya kupigia kura, kuhesabu kura au kujumlishia kura, atatakiwa kabla ya kufanya hivyo kuapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Msimamizi wa Uchaguzi kwa mujibu wa sheria.

### 7.5. Mafunzo kwa Mawakala

Tume itavipatia vyama vya siasa vinavyoshiriki katika uchaguzi vijitabu vya Maelekezo kwa mawakala wa vyama vya siasa. Vyama vitawajibika kutoa mafunzo kwa mawakala kwa gharama zao.

## 7.6. Wajibu wa Mawakala

Wajibu wa mawakala wa upigaji kura ni:-

(i) Kumtambua mpiga kura anayetaka kupiga kura kuwa ndiye mwenye jina lililoandikwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

(ii) Kumwakilisha na kulinda maslahi ya mgombea au wagombea kituoni;

(iii) Kushirikiana na Msimamizi wa Kituo na Msimamizi Msaidizi wa Kituo katika kuhakikisha kwamba mwenendo wa upigaji kura kituoni unazingatia masharti ya Sheria na taratibu zilizowekwa;

(iv) Kujaza Fomu Na. 14 na Na. 16 kituoni, kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi; na

(v) Kukiwakilisha chama chake kwenye zoezi la kuhesabu kura baada ya kukamilika kwa zoezi la upigaji kura kwani wakala wa upigaji ndiye atakuwa wakala wa kuhesabu kura.

Hata hivyo, wakala kutokuwepo au kukataa kusaini fomu zozote anazotakiwa kuzisaini kisheria wakati wa upigaji kura, kuhesabu kura au kujumlisha kura hakutabatilisha kazi yoyote itakayoendeshwa kwa mujibu wa sheria.

Ili waweze kutekeleza kazi hizo kwa ufanisi, Tume inashauri kwamba:-

(i) Vyama vya Siasa viteue mawakala wa upigaji kura wanaowaamini ikiwezekana kutoka miongoni mwa watu waliojiandikisha kuwa wapiga kura kwenye maeneo yenye vituo ambavyo watafanyia kazi.

(ii) Viongozi wa vyama vya siasa wawajibike kuwafundisha mawakala wao taratibu zote za kupiga kura na kuhesabu kura kituoni.

Tume imeandaa vijitabu vya Maelekezo kwa Mawakala wa vyama vya siasa. Wasimamizi wa Uchaguzi watavipatia vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vijitabu hivyo.

Mawakala wa upigaji kura/kuhesabu kura watakaosimamia vituo ambako misafara ya kukusanya masanduku na vifaa vingine itaanza, ndio pia watakaosindikiza na kushuhudia makabidhiano ya vifaa hivyo kwenye kituo cha kujumlishia kura.

## 7.7. Vyama au Wagombea Kushuhudia Ugawaji wa Vifaa

Vifaa vinavyotumika siku ya kupiga kura vitakabidhiwa kwa Wasimamizi wa Vituo vya kupigia kura mbele ya wagombea au wawakilishi wao. Aidha, kila chama kinachoshiriki uchaguzi kitapatiwa orodha kamili ya vifaa muhimu vitakavyotolewa kwa kila kituo.

## 7.8. Wanaoruhusiwa Kuingia Ndani ya Kituo cha Kupigia Kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 63 (2) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi (Sura ya 343) na kifungu cha 63 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, (Sura ya 292), wafuatao ndio wanaoruhusiwa kuingia kwenye kituo cha kupigia kura:-

(i) Msimamizi wa Kituo;
(ii) Wasimamizi Wasaidizi wa Kituo;
(iii) Mawakala wa Upigaji Kura;
(iv) Wapiga Kura kwa ajili ya kupiga kura tu;
(v) Mtu anayemsaidia mpiga kura asiyeweza kupiga kura mwenyewe kwa sababu ya ulemavu au asiyejua kusoma;
(vi) Mtazamaji wa Uchaguzi aliyeidhinishwa na Tume na mwenye kitambulisho maalum kilichotolewa na Tume;
(vii) Mgombea;
(viii) Mjumbe wa Tume;
(ix) Mkurugenzi wa Uchaguzi;
(x) Afisa wa Tume;
(xi) Askari polisi au mtu anayehusika na usalama wa eneo la kujumlishia kura;
(xii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi; na
(xiii) Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa.

**Angalizo**: Watazamaji wa Uchaguzi watapewa vitambulisho maalum kutoka Tume ambavyo vitatumika kuwatambulisha vituoni.

Mtu yeyote ambaye hakutajwa katika sheria kuwa ni miongoni mwa wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura haruhusiwi kuingia kituoni.

## 7.9. Matumizi ya Fomu Na. 15 na Fomu Na. 17

### (i) Fomu Na. 15

Fomu hii hujazwa na mpiga kura ambaye ana malalamiko juu ya mwenendo wa upigaji kura au juu ya utendaji wa Msimamizi wa Kituo au Msimamizi Msaidizi wa Kituo.

### (ii) Fomu Na. 17

Fomu hii hujazwa iwapo Msimamizi wa Kituo, wakala au mgombea atatilia shaka utambulisho wa mpiga kura yeyote anayetaka kupiga kura kuwa hana haki ya kupiga kura au tayari amepiga kura. Msimamizi wa Kituo atampa tahadhari mpiga kura huyo kwamba ni kosa kwa mtu kupiga kura kama hana haki kwa mujibu wa sheria na kwamba, anaweza kushtakiwa mahakamani. Mpiga kura huyo akizidi kudai kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atamtaka kutoa Tamko katika Fomu Na. 17 na kisha atamruhusu kupiga Kura. Mpiga kura akikataa kutoa tamko hataruhusiwa kupiga kura.

Mpiga kura huyo ni sharti awe na Kadi ya Mpiga Kura na awemo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la kituo husika. Fomu Na. 17 sio mbadala wa kadi ya mpiga kura.

## 7.10. Vibali vya Watendaji wa Uchaguzi, Mawakala na Wagombea

### (i) Vibali vya Watendaji wa Uchaguzi na Mawakala (Fomu Na. 18)

Watendaji na mawakala ambao kutokana na majukumu yao katika uchaguzi hawataweza kupiga kura katika vituo walivyojiandikisha watapatiwa vibali maalum kwa kujaziwa Fomu Na. 18 na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ili waruhusiwe kupiga kura katika vituo watakapofanyia kazi.

Endapo mtendaji au wakala anayehusika atapangiwa kufanya kazi nje ya kata aliyojiandikisha hatapiga kura ya Diwani. Kwa halmashauri zenye jimbo zaidi ya moja, mtendaji au wakala atakayepangiwa nje ya jimbo alipojiandikisha hatapiga kura ya Mbunge wala Diwani bali atapiga kura ya Rais tu.

### (ii) Vibali vya Wagombea (Fomu Na. 19)

Wagombea ambao watahitaji kupiga kura katika vituo ambavyo hawakujiandikisha watapatiwa vibali maalum kwa kujaziwa Fomu Na. 19 na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambavyo vitawawezesha kupiga Kura katika kituo chochote katika jimbo au kata yake. Aidha, mgombea Ubunge hataruhusiwa kupiga kura katika jimbo ambalo hakujiandikisha, vivyo hivyo kwa mgombea wa nafasi ya Udiwani katika kata.

**Angalizo:**

1. Ni vema watendaji, mawakala na wagombea watakaopiga kura nje ya vituo walivyojiandikisha wakajulikana mapema ili vibali hivyo viandaliwe na kugawiwa kwa wahusika kabla ya Siku ya Uchaguzi.

2. Kabla mpiga kura aliyetumia Fomu Na. 18 au Fomu Na. 19 hajaondoka, Msimamizi wa Kituo achukue fomu ya mpiga kura huyo aigonge muhuri wa kituo na kuweka katika bahasha Na. 4.

### 7.11. Mambo Yasiyoruhusiwa Kufanyika Siku ya Kupiga Kura

Vyama vya siasa, wafuasi wao na mtu yeyote haruhusiwi kufanya mambo yafuatayo katika siku ya kupiga kura:-

(i) Kufanya Kampeni ya aina yoyote;

(ii) Kuvaa sare au alama za chama, kubeba au kubandika matangazo au kuimba nyimbo za vyama;

(iii) Kuendelea kuwepo katika vituo vya kupigia kura bila ya sababu yoyote;

(iv) Kutumia simu ya kiganjani ndani ya kituo cha kupigia kura/kuhesabia kura na kujumlishia kura isipokuwa kwa watendaji walioruhusiwa kufanya hivyo; na

(v) Kutoa lugha za matusi hadharani kwa watendaji wa uchaguzi katika kituo cha kupigia kura.

# SURA YA NANE

# KUHESABU KURA

## 8.1. Utaratibu wa Kuhesabu Kura

Kwa mujibu wa kifungu cha 70A cha Sheria Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 70A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kura zitahesabiwa katika vituo vya kupigia kura. Mara baada ya kufunga kituo cha kupigia kura, kituo hicho kitageuka kuwa kituo cha kuhesabia kura.

Endapo kutakuwa na sababu za kiusalama au sababu nyingine za msingi Msimamizi wa Kituo baada ya kushauriana na mawakala au kwa kushauriwa na Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi au Mawakala, anaweza kuamua kura zihesabiwe katika kituo kingine cha kupigia kura au sehemu nyingine. Katika kuhesabu kura itahakikishwa kwamba kura zitakazohesabiwa hazichanganywi na hesabu ya kura za vituo vingine.

Wakati wa kuhesabu Kura, endapo itakutwa Kura yoyote imo katika sanduku ambalo sio la Uchaguzi husika, Kura hiyo itahamishwa na kuhesabiwa pamoja na Kura za sanduku la Uchaguzi unaohusika.

Wakati wa kuhesabu kura mambo yafuatayo yatazingatiwa: -

(i) Mawakala wa Upigaji Kura watabadilika na kuwa mawakala wa kuhesabu kura;

(ii) Wasimamizi wa vituo na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya kupigia kura ndiyo watakaohesabu kura;

(iii) Zoezi la kuhesabu kura litafanywa kwa mpangilio kwamba Kura za Rais ndizo zitakazohesabiwa kwanza na zitafuatia kura za Wabunge na mwisho Kura za Madiwani;

(iv) Mawakala au wagombea waliopo wana haki ya kuomba Kura zirudiwe kuhesabiwa hadi mara mbili. Msimamizi wa kituo anaweza kukataa ombi la tatu endapo hesabu ya mara ya kwanza na ya pili zitalingana; na

(v) Wakati wa mchakato wa kuhesabu kura mawakala au wagombea watajaza Fomu Na. 16 katika kila hatua kuonesha kama wameridhika au hawakuridhika na mwenendo mzima wa kuhesabu kura.

**8.2. Wanaoruhusiwa Kuwepo Wakati wa Kuhesabu Kura**

Wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kuhesabia kura ni:-

(i) Msimamizi wa Kituo;

(ii) Msimamizi Msaidizi wa Kituo;

(iii) Mgombea kama atakuwepo;

(iv) Wakala wa Upigaji Kura;

(v) Mtazamaji wa Uchaguzi aliyeidhinishwa na Tume na mwenye kitambulisho maalum kilichotolewa na Tume;

(vi) Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi;

(vii) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(viii) Afisa wa Tume;

(ix) Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa;

(x) Msimamizi wa Uchaguzi;

(xi) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi; na

(xii) Askari polisi au mtu anayehusika na usalama wa mahali pa kuhesabia kura;

**Angalizo**:

1. Watazamaji wa Uchaguzi watapewa vitambulisho maalum kutoka Tume ambavyo vitatumika kuwatambulisha vituoni.
2. Mtu yeyote asiyehusika hataruhusiwa kuwepo katika eneo la kuhesabia kura.

### 8.3. Matokeo ya Uchaguzi katika Kituo

**(i) Fomu za matokeo ya uchaguzi Na. 21A, 21B na 21C SEHEMU A**

Matokeo ya uchaguzi kwa kila kituo yatajazwa kwenye Fomu Na. 21A, 21B, 21C SEHEMU A. Kila fomu itakuwa kwenye kijitabu chake. Mawakala au wagombea watakaokuwepo pamoja na Msimamizi wa Kituo watatakiwa kuweka saini zao. Nakala za fomu za matokeo ya uchaguzi zitabandikwa mahali pa wazi nje ya kituo cha kupigia kura: -

(a) Uchaguzi wa Rais - Fomu Na.21A

(b) Uchaguzi wa Wabunge - Fomu Na.21B

(c) Uchaguzi wa Madiwani – Fomu Na. 21C

Mawakala au wagombea watakaokuwepo wanaweza kupatiwa nakala za Fomu za Matokeo ya Uchaguzi kwa kila Uchaguzi kwa ajili ya kuziwasilisha kwenye vyama vya siasa au wagombea wao.

**(ii) Fomu za Matokeo ya Uchaguzi Na. 21A, 21B na 21C SEHEMU B**

Iwapo kuna kura zenye mgogoro Msimamizi wa Kituo atapaswa kujaza matokeo kama alivyojaza katika kitabu cha matokeo SEHEMU A na kukabidhi kitabu hicho kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atatoa uamuzi wa kura zenye mgogoro na kukamilisha fomu husika. Baada ya Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kutoa uamuzi, mawakala au wagombea waliopo watasaini na Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atawapatia nakala ya fomu husika.

## SURA YA TISA

## KUJUMLISHA KURA

Kwa mujibu wa kanuni ya 64 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2020 na kanuni ya 57 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata baada ya kupokea matokeo ya vituo vyote vya kupigia kura atawajulisha wagombea au vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi siku, mahali na saa ya kujumlisha kura.

### 9.1. Wanaoruhusiwa Kuingia katika Kituo cha Kujumlisha Kura

Wanaoruhusiwa kuwepo wakati wa kujumlisha kura ni:-

(i) Msimamizi wa Uchaguzi;

(ii) Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(iii) Mratibu wa Uchaguzi wa Mkoa;

(iv) Mjumbe wa Tume;

(v) Mkurugenzi wa Uchaguzi;

(vi) Afisa wa Tume;

(vii) Mgombea;

(viii) Wakala wa kujumlisha kura;

(ix) Askari polisi au mtu anayehusika na usalama wa mahali pa kujumlishia Kura; na

(x) Mtazamaji aliyeidhinishwa na Tume na mwenye kitambulisho maalum kilichotolewa na Tume.

**Angalizo**:

Watazamaji wa Uchaguzi watapewa vitambulisho maalum kutoka Tume ambavyo vitatumika kuwatambulisha vituoni.

Mtu yeyote asiyehusika hataruhusiwa kuwepo katika eneo la kuhesabia kura.

### 9.2. Utaratibu wa Kufuata Kabla ya Kuanza Kujumlisha Kura

(i) Kabla ya kuanza kujumlisha kura, Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atatoa maelezo kuhusu utaratibu utakaofuatwa na maadili ambayo waliomo ndani ya kituo cha kujumlisha kura watapaswa kuyafuata;

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atatoa taarifa kuhusu matukio muhimu ambayo ana habari nayo, kuhusu mwenendo wa uchaguzi kwa ujumla;

(iii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atawapatia wagombea nafasi ya kutoa maoni yao kuhusu mwenendo wa uchaguzi; na

(iv) Msimamizi wa Uchaguzi anatakiwa aanze kujumlisha kwanza matokeo ya uchaguzi wa Rais ili yaweze kutumwa Tume kwa haraka.

### 9.3. Utaratibu wa Kufuata Wakati wa Kujumlisha Kura

(i) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atahakikisha kwamba masanduku yote ya kura na Fomu Na. 21A, 21B na 21C sehemu A na sehemu B zimepokelewa.

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata anaruhusiwa kufungua bahasha zifuatazo kwenye kituo cha kujumlisha kura.:-

(a) Bahasha ya Kituo;

(b) Bahasha Na. 1 (Hesabu ya Karatasi za Kura);

(c) Bahasha Na. 3A, 3B, 3C (karatasi za Kura ambazo hazikutumiwa na zilizoharibika); na

(d) Bahasha Na. 5A, 5B, 5C (kura zenye mgogoro).

Baada ya kura zenye mgogoro kufanyiwa uamuzi na Msimamizi wa Uchaguzi, kura halali na kura zilizokataliwa zitaingizwa kwenye bahasha zinazohusika.

**9.4. Kujumlisha Kura za Uchaguzi wa Rais na Wabunge**

Ujumlishaji wa kura kwa Uchaguzi wa Rais na Wabunge utafanyika makao makuu ya halmashauri au jimbo.

Msimamizi wa Uchaguzi atapokea masanduku ya kura fomu za matokeo ya uchaguzi wa Rais na Wabunge kutoka kwenye vituo vyote vya kupigia kura vilivyomo katika Jimbo.

Ujumlishaji wa kura utaanza mara baada ya masanduku yote ya kura na fomu za matokeo kuwasilishwa kwenye kituo cha kujumlishia kura.

Kabla ya kuanza ujumlishaji, Msimamizi wa Uchaguzi atafanya yafuatayo: -

(i) Atatoa taarifa kuhusu matukio muhimu juu ya mwenendo wa uchaguzi;

(ii) Atawapa wagombea au mawakala wao nafasi ya kutoa maoni kuhusiana na uchaguzi;

(iii) Atazitolea uamuzi kura zenye mgogoro na kujaza fomu ya matokeo Na. 21A na 21 B **SEHEMU B**; na

(iv) Atatangaza kwa sauti kubwa matokeo ya kila kituo cha kupigia kura katika Jimbo.

### 9.5. Matokeo ya Uchaguzi wa Rais katika Jimbo

(i) Msimamizi wa Uchaguzi atajumlisha kura za Rais na atakapomaliza atajaza matokeo hayo ya Jimbo katika Fomu Na. 24A. Msimamizi wa Uchaguzi na mawakala au wagombea watakaokuwepo wataweka saini zao kwenye fomu hiyo.

(ii) Msimamizi wa Uchaguzi atampatia wakala au mgombea nakala ya matokeo ya uchaguzi katika jimbo.

(iii) Atabandika nakala ya Fomu Na. 24A mahali pa wazi nje ya kituo cha kujumlishia kura na atatuma mara moja matokeo hayo Tume.

### 9.6. Matokeo ya Uchaguzi wa Wabunge katika Jimbo

Baada ya kukamilisha ujumlishaji wa kura za Rais, Msimamizi wa Uchaguzi atafanya ujumlishaji wa kura za Wabunge hatua kwa hatua na atakapomaliza ujumlishaji huo atafanya yafuatayo: -

(i) Atajaza matokeo ya uchaguzi wa Ubunge kwenye Fomu Na. 24B. Msimamizi wa Uchaguzi na mawakala au wagombea watakaokuwepo wataweka saini zao;

(ii) Atamtangaza mgombea aliyeshinda;

(iii) Atabandika nakala ya fomu ya matokeo ya uchaguzi katika mahali pa wazi nje ya kituo cha kujumlishia kura;

(iv) Atampatia hati ya kuchaguliwa mgombea aliyeshinda; na

(v) Atawasilisha mara moja matokeo hayo Tume.

## 9.7. Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani katika Kata

Ujumlishaji wa kura kwa uchaguzi wa Madiwani utafanyika kwenye kata. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata atapokea masanduku ya kura na fomu za matokeo ya uchaguzi kutoka kwenye vituo vya kupigia kura.

Ujumlishaji wa kura utaanza mara baada ya masanduku yote ya kura na fomu za matokeo kuwasilishwa kwenye kituo cha kujumlisha kura.

Baada ya kukamilisha ujumlishaji wa kura, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata atafanya yafuatayo:-

(i) Atajaza fomu ya matokeo Na. 24C;
(ii) Atamtangaza mgombea aliyeshinda;
(iii) Atabandika nakala ya fomu ya matokeo ya uchaguzi katika ubao wa matangazo;
(iv) Atampatia hati ya kuchaguliwa mgombea Udiwani aliyeshinda; na
(v) Atawasilisha mara moja matokeo hayo kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

## 9.8. Maombi ya Wakala au Mgombea Kurudia Kuhesabu Kura

Kabla ya kuaza kujumlisha kura wakala au mgombea anaweza kuomba kuhesabiwa upya kwa kura za baadhi ya vituo, ikiwa usahihi wa matokeo ya kituo au vituo hivyo ulipingwa na wakala au mgombea wakati wa kuhesabu kura katika kituo cha kuhesabia kura. Wakala au Mgombea hataruhusiwa kuomba kuhesabiwa upya kwa kura za vituo vyote.

Mgombea au wakala anaweza kuomba kwa Msimamizi wa Uchaguzi au Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata kuhakiki usahihi wa ujumlishaji wa kura.

**9.9. Kujumlisha Kura za Uchaguzi wa Rais kwa Nchi Nzima**

Tume ndiyo itakayojumlisha kura za nchi nzima za Uchaguzi wa Rais. Tume itawajulisha vyama vya siasa na wagombea siku, mahali na saa itakapofanya ujumlishaji wa kura za wagombea wa kiti cha Rais. Aidha, baada ya Tume kupokea matokeo ya awali kutoka kwa Wasimamizi wa Uchaguzi na kuyahakiki itatangaza matokeo ya uchaguzi kwa kila Jimbo.

**9.10. Yanayotakiwa Kufanywa na Tume Kabla ya Kuanza Ujumlishaji wa Kura za Rais**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kabla ya kuanza zoezi la kujumlisha itatakiwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa taarifa kuhusu matukio muhimu;

(ii) Kuwapa nafasi wagombea kutoa maoni yao kuhusiana na uchaguzi; na

(iii) Kutangaza kwa sauti inayosikika kwa watu wote matokeo ya uchaguzi wa Rais kutoka katika majimbo yote ya uchaguzi.

Tume itajumlisha matokeo ya kura za majimbo yote na itakapomaliza ujumlishaji itajaza matokeo ya kila mgombea katika Fomu Na. 27. Mwenyekiti wa Tume, wagombea au mawakala watakaokuwepo wataweka saini zao kwenye fomu hiyo.

### 9.11. Kumtangaza Mshindi wa Kiti cha Rais

Tume itatangaza idadi ya kura alizopata kila mgombea. Mgombea aliyepata kura nyingi zaidi atatangazwa kuwa mshindi wa kiti cha Rais na Tume itampatia Hati ya Kuchaguliwa.

# SURA YA KUMI

# UTEUZI WA WABUNGE NA MADIWANI WA VITI MAALUM VYA WANAWAKE

## 10.1. Wabunge wa Viti Maalum vya Wanawake

Kwa mujibu wa ibara ya 66 na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 vyama vya siasa vitapendekeza kwa Tume majina ya wanawake ambao Tume inaweza kuwatangaza kuwa Wabunge kama ikiridhika kwamba wana sifa zinazostahili.

Tume inatakiwa kutangaza majina ya wanawake kwa idadi ya asilimia arobaini (40%) ya Wabunge wote kwa ajili ya Viti Maalumu vya wanawake. Mgawanyo huo utazingatia uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata katika uchaguzi wa Bunge.

Endapo mgombea Ubunge amepita bila kupingwa, kura za mgombea Kiti cha Rais wa chama cha Mbunge katika jimbo husika zitachukuliwa kuwa ndizo kura halali za Mbunge huyo. Kama chama hakina mgombea wa kiti cha Rais, asilimia hamsini na moja (51%) ya idadi ya wapiga kura walioandikishwa itachukuliwa kuwa ndio kura halali za Mbunge wa chama husika.

Hata hivyo, chama kinaweza kupata nafasi ya kiti maalum cha Mbunge mwanamke endapo kimepata angalau asilimia tano (5%) ya kura zote halali za uchaguzi wa Wabunge.

Ili kuwapata Wabunge Wanawake wa Viti Maalum, vyama vya siasa vina wajibu ufuatao:-

(i) Kupendekeza majina ya wanawake kwa idadi itakayopendekezwa na Tume kwa mujibu wa ibara ya 66 (b) na ibara ya 78 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kwa mpangilio wa upendeleo (*order of preference*) na kuituma Tume siku thelathini (30) kabla ya uchaguzi.

(ii) Kuhakikisha kwamba wanaopendekezwa wanajaza fomu za uteuzi Na. 8D na kuziwasilisha pamoja na picha nne (4) zenye ukubwa sawa na picha ya pasi ya kusafiria (*passport size*). Picha hizo ziwe zimepigwa ndani ya miezi mitatu.

(iii) Wanawake watakaopendekezwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum hawatakiwi kuweka dhamana ya shilingi elfu hamsini (50,000/=).

**10.2. Madiwani wa Viti Maalum vya Wanawake**

Viti maalum vya wanawake kwa upande wa Madiwani vinapatikana kwa kuzingatia uwiano wa idadi ya viti ambavyo kila chama kimepata katika uchaguzi wa Madiwani katika Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya.

Viti hivyo ni theluthi moja ya jumla ya Madiwani wa kuchaguliwa na Wabunge wanaowakilisha Majimbo ya Uchaguzi katika eneo husika.

Ili kutekeleza hayo, vyama vya siasa vina wajibu ufuatao:-

(i) Kupendekeza majina ya wanawake ambao watakuwa ni theluthi moja ya jumla ya Madiwani wote wanaowakilisha Kata na Wabunge wanaowakilisha Majimbo ya Uchaguzi. Orodha ya majina hayo

iliyopangwa kwa upendeleo (*order of preference*) ipelekwe Tume siku thelathini (30) kabla ya Siku ya Upigaji Kura.

(ii) Kuhakikisha kwamba vinapendekeza wanawake wenye sifa za kuwa Madiwani.

(iii) Kuhakikisha kuwa wanawake wanaopendekezwa kuwa Madiwani wa viti maalum vya wanawake wanajaza Fomu za Uteuzi Na. 8E na kuambatisha picha nne (4) zenye ukubwa sawa na picha ya pasi ya kusafiria (*passport size*).

Wanawake watakaopendekezwa hawatakiwi kuweka dhamana ya shilingi elfu tano (5,000/=).

**Angalizo:**

Vyama vya siasa vinakumbushwa kuwasilisha Tume orodha ya mapendekezo ya majina ya Wabunge na Madiwani wa Viti Maalum vya wanawake siku thelathini (30) kabla ya siku ya uchaguzi.

## SURA YA KUMI NA MOJA

## USHAURI KWA VYAMA VYA SIASA

Tume inatoa ushauri ufuatao: -

(i) Vyama vya siasa vihakikishe vinatimiza wajibu wao kama ilivyoelezwa katika Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni za Uchaguzi, Maadili ya Uchaguzi na Maelekezo ya Tume.

(ii) Vyama vinakumbushwa kwa mujibu wa kifungu cha 85 cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 na kifungu cha 86 cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, kwamba, kutokuwepo kwa wakala au mgombea mahali ambapo wanaruhusiwa kuwepo katika hatua yoyote ya uchaguzi, hakutazuia wala kubatilisha shughuli ya uchaguzi iliyofanywa kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, vyama vya siasa vinatakiwa kufahamu kwamba:-

(a) Saa ya kuanza upigaji kura itakapofika, hata kama wakala hayupo zoezi la kupiga kura litaanza;

(b) Saa ya kujumlisha kura itakapofika, hata kama wakala hayupo zoezi la kujumlisha kura litaendelea; na

(c) Saa ya kutangaza matokeo itakapofika, hata kama wakala hayupo, matokeo yatatangazwa kwa mujibu wa Sheria.

(iii) Vyama vya siasa viwaelimishe wagombea na mawakala wao kuhusu taratibu zote za uchaguzi kwa gharama zao.

(iv) Vyama vya siasa viwahamasishe wanachama wao na wananchi kwa ujumla umuhimu wa kujitokeza na kushiriki kwenye uchaguzi.

(v) Vyama vya siasa viwaelimishe wapiga kura kuwa baada ya kumaliza kupiga kura warudi nyumbani na wasikaribie eneo la upigaji kura.